Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 21 Aprili, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

## *D U A*

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza shughuli zetu hizi za Mkutano wa Kumi na Tano, mtakumbuka kwamba tulifikwa na msiba wa Mwenzetu, Mbunge wa Busanda Mheshimiwa Faustin Rwilomba, ambaye alifariki na tulishiriki katika mazishi. Kwa hiyo, kama ilivyo kawaida nakuombeni kabla hatujaanza shughuli za leo tusimame kwa dakika moja kumkumbuka marehemu

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kukumbuka kifo cha Mheshimiwa Faustin Rwilomba)*

**SPIKA**: Ahsanteni sana, tunamwomba Mwenyezi Mungu aweze kuiweka roho ya Mwenzetu Faustin Rwilomba mahali pema peponi, Amin.

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Bunge letu hili lilipitisha Miswada saba ya Sheria ya Serikali kama ifuatavyo:-

*The Public Health Bill 2009, The Standards Bill, 2009, The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2009, Tanzania Trade Development Authority Bill, 2009, The Wildlife Conservation Bill, 2009, The Supplementary Appropriation Bill,2008/2009* na *Political Parties Bill, 2009*.

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya kupitishwa na Bunge na baadaye kupitia katika hatua zake zote za uchapishaji, Miswada hiyo ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ili kuweza kupata kibali chake kwa mujibu wa Katiba.

Waheshimiwa Wabunge nafurahi kuwaarifu kwamba tayari Mheshimiwa Rais amekwishatoa kibali chake na sasa Miswada hiyo ni Sheria za nchi yetu kama ifuatavyo:-

*The Public Health Act, 2009* utakuwa ni namba moja wa 2009, *The Standards Act,2009* ni namba mbili wa mwaka 2009, *The Written Laws Miscellaneous Amendment Act*, 2009 sasa ni sheria namba tatu ya mwaka 2009, *The Tanzania Trade Development Authority Act, 2009* ni sheria namba nne ya mwaka 2009, *The Wildlife Conservation Act*, 2009, sasa ni sheria namba tano ya mwaka 2009, *The Supplementary Appropriation Act*, 2008/2009 ni sheria namba sita ya mwaka 2009 na *The Political Parties Act*, 2009 sasa ni Sheria ya saba ya mwaka 2009, Ahsante sana.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Taarifa ya matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge uliopita.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge kabla sijawaruhusu mwuulize maswali nasikitika kwamba swali namba mbili na swali namba kumi na tatu majibu yake hayakukamilika kwa sababu maswali yote mawili yamegusa Wizara tofauti tofauti. Kwa mfano swali la pili linahusu Ofisi ya Waziri Mkuu na pia Wizara ya Miundombinu, na swali namba kumi na tatu linahusisha Wizara ya Ardhi na Kilimo. Kwa hiyo, tutajitahidi yaweze kujibiwa katika kipindi hiki hiki cha Mkutano wa Kumi na Tano.

Waheshimiwa Wabunge baada ya taarifa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mifenesini, kwa swali la Kwanza.

Na.1

**CDA Kuwa na Mipango ya Kukidhi Maombi ya Viwanja.**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa imeonekana dhahiri wapo wananchi wengi wenye nia ya kujenga nyumba za kuishi na biashara katika Manispaa ya Dodoma lakini inaonekana mamlaka ya *CDA* haijajiandaa vyema kukidhi haja ya waombaji:-

Je, Serikali itahamasisha vipi Mamlaka kupanga mipango madhubuti ya kukidhi mahitaji ya waombaji wa viwanja?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mifenisini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji wa Mji wa Dodoma imekuwa katika miaka ya hivi karibuni kutokana na ujio wa taasisi kadhaa za elimu ya juu, kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana na upanuzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) na Chuo cha Mipango kuwa Vyuo Vikuu.

Taasisi hizi zimesababisha ongezeko kubwa la watu ambao wanahitaji nyumba za kuishi na za biashara na uhitaji wa viwanja kwa ajili ya shughuli nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Dodoma *(CDA)* ni chombo cha Serikali chenye jukumu muhimu la kuandaa mipango ya ujenzi wa Mji Mkuu ikiwa ni pamoja na kupanga , kupima na kumilikisha viwanja katika eneo la Makao Makuu.katika kujiandaa vyema kukidhi mahitaji ya waombaji wa viwanja, Mamlaka imefanya yafuatayo:-

(i) Imegharamia mradi mkubwa wa upigaji picha za ndege na utayarishaji wa ramani za msingi (*base maps)* zinazohitajika katika kutayarisha michoro ya kimpango Miji kwa eneo lote la Mji lenye ukubwa wa hekta 260,790.

(ii) Mamlaka imeendelea kupanga viwanja kwenye maeneo mapya mbalimbali, kwa mfano, Mamlaka imetayarisha mpango wa viwanja 20,800 katika maeneo yafuatayo vinavyongojea kupimwa:- Iyumbu viwanja 4000, Mkalama 1,300, Mkonze 3000, Nzuguni 3000, Ndachi 4000, Ntyuka 3000, Msalato 2500 pamoja na eneo la uwekezaji wa ujenzi wa maghorofa *Real Estate* la Ndejengwa ambapo hekta 580 zimepangwa kupimwa viwanja vikubwa blocks vyenye ukubwa na kati ya Hekta 1.5 hadi hekta 12.

(iii) Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeandaa ramani, mpango wa Mji mpya wa Iyumbu (*New Town*), utakaojumuisha maeneo yanayokizunguka Chuo Kikuu cha Dodoma utakaotosheleza mahitaji ya huduma zote.

(iv) Serikali imeitaka mamlaka kuwatumia pia Wakandarasi (Wapima binafsi) ili kuongeza kasi ya upimaji.

Mheshimiwa Spika, kikwazo kikubwa katika upimaji viwanja ambavyo tayari vimechorwa, ni ukosefu wa fedha za kutosha za kulipia fidia ya utwaaji wa ardhi katika maeneo husika na kisha uwezeshaji wa upimaji wa viwanja.

Hata hivyo ili kuihamasisha Mamlaka, Serikali imejipanga kuiimarisha mamlaka kiutawala na kifedha kutoka bajeti ya Serikali na inaangalia pia uwezekano wa viwanja vingi vya ukubwa mbalimbali kufuatana na uwezo wa mtaji huo na wakati huo huo kuanzisha mfuko wa upimaji viwanja *Plot Development Revolving Fund* utakaokuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeipa Mamlaka wigo, kulingana na Sheria ya Kuanzishwa kwake, kuweza kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine ya kuanzishwa kwake, kuweza kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine vya fedha nje ya bajeti ya Serikali kama vile mabenki au Mashirika ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kutimiza majukumu yake ya msingi kikamilifu na kuweza kurudisha mikopo hiyo kwa kuuza viwanja husika kwa waombaji.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kumwuuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi unapoanzisha mamlaka yeyote, unakusudia kuwa watu wa hapo wenyewe hasa kuweza kujenga nyumba za kuishi pamoja na za biashara, inaonekana kazi kubwa inayofanywa ya kupima viwanja lakini bado bei ya viwanja ni kubwa kama ilivyoonekana kama viwanja vilivyouzwa hivi karibuni katika eneo la Mirembe, ni lini sasa Mamlaka hii itafikiria namna ya kupunguza bei ya viwanja ili Wakazi waliowengi wawe na uwezo wa kununua viwanja hivi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, inawezekana bei ya viwanja ni kubwa kwa Mtanzania wa kawaida lakini ukiangalia katika hali halisi ya uandaaji wa viwanja hivyo, kinacholipwa na mwombaji wa kiwanja ni gharama ya upimaji tu wala si huduma zingine kama vile barabara, maji na umeme kwa vile Mamlaka haipati ruzuku kubwa kutoka Serikalini, inachofanya ni kuuza hivyo viwanja kwa bei ambayo inalingana na gharama ya upimaji.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wana uwezo wa chini kabisa kuna maeneo ambapo viwanja ni kati la laki moja na laki mbili na maeneo haya ni Nzunguni upande wa kushoto wa barabara inayoenda Dar es Salaam.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma mara nyingi wanakuwa na ugomvi na *CDA* katika suala zima la kung'ang'ania ugawaji wa viwanja ikiwa ni pamoja na ujenzi holela wanaoufanya wananchi.

Je Serikali ni kwa nini ikiwa inatambua kuwa imeipatia Mamlaka ya *CDA* mamlaka kamili ya kuendeleza Mji wa Dodoma. Kwa nini isiisaidie mapema kuhakikisha kwamba wao ndiyo wanakuwa na nguvu inapofika suala la kuvunja nyumba zilizojengwa holela itekelezwe maana Dodoma si mahali pa kujenga holela kwa vile sehemu kubwa ya Mji imepimwa. Vile vile kuhakikisha kuwa inatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali inachelewa, au kuna kigugumizi fulani?

**SPIKA**: Naliona swali ni jipya linastahili kuulizwa rasmi kama swali.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika nakushukuru, Mheshimiwa Waziri wakati wa majibu yake alisema kwamba ni kweli viwanja hivi kwa watu wa kawaida bei yake iko juu. Hivi kwani Serikali inawakusudia akina nani, walengwa hasa ni akina nani, ni watu maalum wala si watu wa kawaida? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, katika kugawa viwanja tunawalenga watu wengi sana na ndiyo maana viwanja vinauzwa kwa bei tofauti. Tuchukue eneo ambalo tuliuza viwanja wakati wa Mkutano wa Bunge uliopita, eneo la Itega. Pale kuna eneo la makazi ambapo walengwa ni wale ambao watahitaji eneo la makazi mapana, *very Low Density* gharama yake ni kubwa. Eneo la flats maghorofa kwa watu ambao wanapenda kuwa na *apartments* kwa ajili ya kupangisha watu wenye uwezo mkubwa, na kadhalika. Wengine wanahitaji maeneo kwa ajili ya viwanda, taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi hata Mji wenyewe unapangwa kutegemeana na walengwa wa aina mbalimbali watakaotumia maeneo ya Mji.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Dodoma Serikali ilishakiri kwamba kuna mapungufu na iliahidi kuleta Muswada kwenye Bunge hili, nilikuwa naomba Waziri alieleze Bunge hili ni lini Muswada huo utaletwa Bungeni ili kuondoa Migongano kati ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** MhMamlaka ya Makao Makuu ina mapungufu makubwa na imepitwa na wakati, lakini naamini pia Mheshimiwa Lubeleje ni Mbunge Mkongwe wa Muda mrefu, anafahamu mchakato wa namna ya kuleta Miswada Bungeni. Mchakato wa kuleta sheria mpya ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma umefikia hatua nzuri na kwa sasa uko katika ngazi ambayo inaitwa *IMTC*. Ngazi ya Makatibu Wakuu na ikifika pale italetwa kwenye Baraza la Mawaziri na Baraza la Mawaziri likiafiki maudhui yote ndiyo Muswada utaandaliwa na sheria hiyo itakapokamilika nina hakika matatizo mengi yatatatuliwa ikiwa ni pamoja na mgongano wa madaraka na mamlaka kati ya Madiwani wa Manispaa ya Dodoma na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Lubeleje, Wabunge na wananchi wa Dodoma wavute Subira wakati wowote kuanzia sasa tutawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Ustawishaji wa Makao Nakuu. Dodoma.

Na. 3

**Upungufu wa Watumishi wa Afya**

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Kwa kuwa, kero mojawapo inayowakera wananchi ni upungufu mkubwa sana wa watumishi kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; na kwa kuwa ni wajibu wa mwajiri kumlipa mwajiriwa mshahara wake anaostahili; na kwa kuwa ni kwa zaidi ya miaka kumi sasa tangu kuwepo kada ya Wauguzi wenye Shahada:-

(a) Je, hadi leo kuna *Scheme of Service* ya Wauguzi?

(b) Je, Muuguzi mwenye kiwango cha elimu ya *Diploma* na mwenye Shahada wanastahili kulipwa kiasi gani cha mshahara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali lka Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu, Mbunge wa Viti Maaluum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miundo ya utumishi ya kada zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inayotumika sasa iliidhinishwa mwaka 2002 kwa Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 23. Katika miundo hiyo ipo kada ya Wauguzi. Hata hivyo, kada ya Wauguzi iliyopo katika Waraka huo ni ya Wauguzi wenye Stashahada.

(b)

Ili kwenda na mabadiliko mbali mbali yanayotokea, miundo hiyo sasa imehuishwa ili pamoja na mambo mengine ni kutambua na kuzingatia sifa za kitalaam ambazo hapo awali hazikuwepo. Miundo hiyo ni pamoja na Shahada, Maafisa Mazingira wenye Shahada na kadhalika.

Kwa mujibu wa taratibu, miundo hiyo inapaswa kuidhinishwa na Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini kabla ya kuanza kutumika. Baraza hili linatarajia kukutana mwezi Mei, 2009 ambapo miundo ya kada zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itawasilishwa ili uweze kupitishwa ukiwemo muundo wa utumishi wa Wauguzi wenye Shahada.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu awali katika sehemu (a) ya swali la Mheshimiwa Mushashu, Serikali haikuwa na muundo wa Wauguzi wenye Shahada kwa kuwa Wauguzi wenye sifa hizo hawakuwepo. Hivyo kwa sasa Wauguzi wenye Shahada wanaendelea kulipwa mshahara katika ngazi ya *TGHS B1*. Hata hivyo, kwa kutambua kuwepo Wauguzi wenye elimu ya Shahada, muundo wa maendeleo ya utumishi wa kada ya Wauguzi utakapopitishwa utakuwa na ngazi ya kuanzia mishahara ya *TGHS C1*. *(Makofi)*

**MHE. BENADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa, ni haki ya mwajiriwa kulipwa mshahara anaostahili, na kwa kuwa ni wajibu wa mwajiri kuhakikisha kwamba anamlipa mwajiriwa mshahara unaostahili lakini sasa hivi ni zaidi ya miaka kumi tangu iwepo kada ya manesi wenye Digrii lakini wanaendelea kulipwa Mshahara wa *Diploma.*

Je, Waziri anawapa matumaini gani kwa sababu sasa hivi wanamsikiliza. Ni lini watakuwa wamelipwa mshahara stahili ambao ni mshahara wa digrii, tunaomba awape muda.?

(ii) Kwa kuwa, wauguzi kote nchini walioajiriwa wenye Digrii na Wizara ya Afya Mkoa wa Kagera, Dar es Salaam hata pale Muhimbili na popote hadi leo hawajalipwa mishahara katika kipindi cha zaidi ya miezi sita, sijui ni kwa nini hawajalipwa na Serikali inafikiri wanaishije na ni lini itakuwa wamelipwa mshahara wao hata ule wa Diploma hawajaanza kulipwa.*(Makofi*)

(iii)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba Baraza la Wafanyakazi ambalo litajadili Muundo wa Watumishi wa Kada za afya litakaa mwezi Mei, 2009. Napenda nimhakikishie Mbunge kwamba Mishahara wanayostahili wauguzi wenye shahada itaanza kulipwa mwezi Julai, 2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Watumishi wa afya ambao wameajiriwa na ambao hawajalipwa mishahara mpaka sasa hivi, kwanza napenda nisikitike kwamba nalisikia kwa mara ya kwanza kwamba wapo watumishi ambao wameajiriwa tangu kipindi hicho ambao hawajalipwa mishahara, kwa taarifa ambazo nimetoka nazo ofisini kwangu watumishi wote ambao walikuwa hawajaingia katika *payroll* waliingia mwezi Machi na kwa sasa hivi hakuna Mtumishi ambaye taarifa zake zimefika katika ofisi zetu na ambaye hajaingia kwenye *payroll.*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafsi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa moja ya sababu ambayo wataalamu wetu wengi ambao wanafundishwa kwa pesa za Serikali wamekuwa wakiacha kazi Serikalini na kwenda kwenye taasisi binafsi hata nchi za nje ni pamoja na mishahara midogo. Lakini pia na marupurupu ambayo hayatoshelezi, watalaamu wengi ambao wamekuwa wakiondoka ni pamoja na wauguzi, Je, Mheshimiwa Waziri anawaambiaje Wauguzi hawa na watalaamu wengine ambao wamekuwa wakiondoka kwa sababu za kutokuwa na mishahara ya kutosha na marupu rupu kwamba marekebisho ambayo yanaendelea Serikalini yatakuwa bora zaidi kuliko yale ya sekta binafsi ili watalaamu tunawasomesha kwa pesa nyingi za Serikalini wasiweze kuondoka na kwa maana hiyo wawatumikie Watanzania?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**: Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie kwamba sasa hivi kwa kiasi kikubwa Serikali imejitahidi katika kuongeza mishara ya watumishi hasa kada za afya, na napenda nimhakikishie kwamba sasa hivi taasisi nyingi za binafsi haziwezi tena

kuchukua watumishi wa kada za afya kutokana na viwango vipya vya mishahara ambavyo vinalipwa na Serikali na sasa hivi kumekuwa na malalamiko kutoka taasisi za dini hasa hospitali za dini kwamba mishahara inayolipwa na Serikali ni mikubwa ukilingalisha na wanayolipa wao na wengi wamekuwa wakiiomba Serikali iwasaidie katika kulipa mishahara hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie kwamba wanaokwenda nje ya nchi wanakuwa na malengo mengi zaidi kuliko hilo la mishahara lakini kwa ndani hakuna mtumishi wa kada ya afya sasa hivi ambaye anaondoka katika Serikali akaenda katika sekta binafsi na hata wanaostaafu hakuna anayeenda kufanya kazi za mikataba katika taasisi binafsi wote wanaomba mikataba Serikalini. Kwa hiyo, sasa hivi kwa kweli hata sisi tunapata moyo kwamba watumishi wameanza kubaki katika sekta ya afya.

Na. 4

**Wizi wa Nyaraka Muhimu za Serikali**

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni umezuka mtindo wa wizi wa nyaraka muhimu za Serikali na Taasisi zake jambo ambalo ni la kutisha na hatari sana:-

(a) Je, kuna watu wowote waliokamatwa kati ya mwezi Januari hadi Disemba mwaka 2008, na kama wapo ni wangapi na wamechukuliwa hatua gani za kinidhamu?

(b) Je, ni jihada gani za makusudi zimechukuliwa kuzuia hujuma hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa hivi sasa lipo tatizo la upatikanaji wa nyaraka muhimu za Serikali na Taasisi zake katika maeneo au mikononi mwa watu wasiohusika na kutumika isivyostahiki.

Tatizo hili haliwezi kupuuzwa, na hivyo halina budi kufanyiwa kazi kwa kina ili kudhibiti matumizi mabaya ya nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nyaraka za Serikali ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria mbalimbali za nchi. Sheria hizo ni pamoja na sheria ya usalama wa Taifa Na. 3 ya Mwaka 1970, Sheria ya kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, sheria ya Utumishi ya Umma Na. 8 ya mwaka 2002, na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma. Sheria hizi zinaainisha mgawanyo wa majukumu baina ya vyombo mbalimbali vya dola na unatoa madaraka ya kuwakamata na kuwafikisha mbele ya sheria, watuhumiwa wa wizi na Nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na vyombo vya dola, ofisi yangu inaendelea kufanya uchunguzi wa kubaini chanzo na wahusika wa wizi wa nyaraka za Serikali na endapo mtu yeyote atakamatwa atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

(b)Mheshimiwa Spika, ofisi yangu imechukua hatua mbalimbali za kuzuia hujuma hizo kama ifuatavyo:-

(1)Kuanzia mwaka 1997 Serikali imeongeza kiwango cha elimu kwa kada ya Watunza Kumbukumbu na kuboresha mafunzo yao kwa kiwango cha Cheti na stashahada ya Utunzaji Kumbukumbu.

(2)Kutunga sheria Mpya ya Utunzaji kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Namba 3 ya mwaka 2002 ambayo inatilia Mkazo umuhimu wa Utunzaji kumbukumbu kwa mamlaka mbalimbali.

(3) Kuweka mfumo mpya wa utunzaji kumbukumbu unaodhibiti ufunguaji na utekelezaji wa majadala na nyaraka kiholela.

(4) Kuanzia mwaka 2005 hadi 2007, Serikali ilitoa mafunzo maalum kwa watunza kumbukumbu 900 kutoka Wizara, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Idara zinazojitegemea, ofisi za Wakuu wa Wilaya, na Halmashauri za Wilaya zote nchini.

(5) Serikali iliandaa na kusambaza katika ofisi zote za Serikali waraka maalumu wenye Kumb. BD.45/239/01/B89 wa tarehe 26 Novemba, 2001, wenye madhumuni ya kudhibiti matumizi ya kumbukumbu za *electronic (E-mails).*

(6) Serikali pia ilisambaza kwa mamlaka zote, waraka Maalumu wenye Kumb. Na. C/CA/213/273/01/124 wa tarehe 11 Oktoba , 2007 kwa lengo la kuhimiza usimamizi wa karibu wa Nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa taasisi zote za Umma kuwa makini hasa kwa kuzingatia mazingira ya sasa ambapo kuna matumizi makubwa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(TEKNOHAMA)* katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, kwani ni njia rahisi kwa watumishi wasio waaminifu kuvujisha nyaraka za Serikali.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini hakulifanyia haki swali langu la kwanza (a) hakulijibu ambalo linasomeka. Je, kuna watu wowote waliokamatwa kati ya mwezi Januari hadi Disemba 2008 na kama wapo ni wangapi na wamechukuliwa hatua gani za kinidhamu?

**SPIKA**: Nina hakika Mheshimiwa Waziri atakuwa na maelezo tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, tangu kipindi ambacho amekionyesha ni kwamba mpaka sasa hivi hakuna ambao tumewakamata kwa ushahidi, wengi tumekuwa tukiwahisia kwa hiyo bado tunaendelea kuwachunguza na tumewabadilisha maeneo yale ambayo tulikuwa tunaona ni nyeti na ambayo nyaraka nyingi zimekuwa zikivuja, kwa hiyo bado tunaendelea na uchunguzi hatuna ambayo tumewashika kwa ushahidi kabisa kwamba ndiyo wanaovujisha nyaraka za Serikali. (*Makofi*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi moja ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali la msingi ameorodhesha sheria ambazo zinapaswa kusimamia suala zima la siri za Serikali. Lakini vile vile tunazo sheria za kinga na haki za Bunge.

Je, Mbunge kwa kutumia sheria hiyo ya Haki na Kinga za Bunge akiibuka Bungeni na nyaraka za Serikali za siri ambazo ameziiba, ni sheria ipi itakayofanya kazi?(*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, nadhani sheria ya kinga iliyopo haimkingi Mbunge kuiba nyaraka za Serikali na wala haimkingi na wizi Mbunge yeyote katika sheria yeyote ya hizo ulizozungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wengi wa Wabunge walioonekana na nyaraka za Serikali walikuwa wakizitumia kwa misingi sana ya kutaka kujijengea sifa kisiasa ambazo sisi hatukutaka kuwakamata kwa sababu tulikuwa tunajua dhumuni lao na pia hatukuona kama kungekuwa na athari sana.

Lakini lengo lao kubwa ilikuwa ni kutaka kujijengea sifa za kisiasa. Kwa hiyo hiyo kinga haiwakingi lakini tuliamua kuwaachia. (*Kicheko*)

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kuniona, swali langu linafanana na la mwuuliza swali aliyepita.

Kwa kuwa hivi karibuni tumewasuhudia Wabunge wenzetu humu ndani wakitumia nyaraka za Serikali ambazo ni siri, hivi bado tunahitaji utafiti juu ya hilo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema katika swali la kwanza la nyongeza kwamba kwanza hawana kinga ya kuiba nyaraka za Serikali lakini pili ni kweli tunahitaji utafiti ili tujue wanaowapatia hawa na wanawapatia kwa malengo gani, baadhi yao tumeanza kuwafuatilia kwa karibu kwa sababu tunazo taarifa kwamba wengi wa nyaraka hizo wanazinunua wala hawazipati bure kutoka kwa hawa wanaowapa na tunaendelea kuwafuatilia.

Ninachotaka kusema na nitoe wito kwamba tunaomba wasirudie, tumelizungumza hapa tumelisikia wakiendelea sheria itachukua nafasi yake na wizi wa nyaraka wamo humu ndani na wananisikia(*Kicheko*)

Na. 5

**Kutambua na Kuboresha Maslahi ya Mashujaa wa Vita wa Tanzania**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania hufanya maadhimisho ya siku ya Mashujaa kila mwaka ikiwa ni ishara ya kumbukumbu ya kuwaenzi kwa mchango wao mkubwa kwa Taifa; na kwa kuwa, Mashujaa wengi ni wastaafu, wengine walipata ulemavu wa kudumu na wengine walipoteza maisha yao vitani:-

(a) Je, Serikali inajua idadi halisi ya mashujaa waliopo hai nchini?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa Mashujaa hao hali zao za maisha ni mbaya na maslahi yao hayajaboreshwa kwa muda mrefu?

(c) Je, hayo ndiyo malipo ya mchango wao kwa Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, linafahamu wanajeshi walioshiriki vita. Hata hivyo baada ya kumalizika vita wanajeshi walioshiriki vita kufikia umri wa kustaafu, hurejea makwao. Baada ya hapo inakuwa vigumu kujua kila shujaa alipo kwa sababu mashujaa hao hawalazimiki kukaa makwao isipokuwa kwa wale maafisa walio katika mkataba wa Jeshi la akiba ambao wameacha anwani zao Makao Makuu ya Jeshi.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa wastaafu wengi wakiwemo mashujaa wa vita wanapokea pensheni ambazo hazikidhi hali ngumu ya maisha iliyopo hivi sasa. Aidha, hatua zimechukuliwa na Serikali kupandisha kiwango cha chini cha pensheni kufikia Tsh. 50,000/= kutoka Tsh. 20,000/= za sasa.

(C) Mheshimiwa Spika, hakuna malipo yanayofanana na kazi nzuri iliyofanywa na Mashujaa wetu kwa nchi yao, hivyo Serikali itaendelea kuwaenzi na kuboresha maslahi ya waliopo kazini na wastaafu mara kwa mara.maisha ya mwanadamu hayawezi kuthaminishwa kwa fedha, ndiyo sababu Amiri Jeshi Mkuu alitoa tamko kuwa “Taifa litakachoweza kuwalipa ni Asante.”

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu yasiyoridhisha kwa wastaafu na wahanga wa vita nina maswali mawili ya nyongeza.

(a)Je. Serikali haioni sasa kuwa kuna haja ya kuweka kiwango maalumu cha wastaafu wahanga wa vita kutoka shilingi hamsini elfu mpaka kufikia laki mbili kwani wengi wao wakiwa hawana viungo.

(b)Je Serikali inatoa kauli gani kwa familia za marehemu ambao mashujaa hao wameshakufa lakini familia hizo zinatangatanga na hawajui la kufanya?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimefurahishwa na swali lake zuri linaloridhisha, pili swali lake la kwanza linahusu kiwango kuongezwa kutoka shilingi elfu hamsini mpaka shilingi laki mbili, wazo lake ni zuri sana na mara Serikali itakapopata uwezo itafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Serikali inatoa kauli gani kwa marehemu walioshiriki katika vita, utata wa swali hili ni kwamba vita hasa inayozungumziwa ni ya Idd Amin ya mwaka 1979.

Kwa hiyo hata unapoongelea watoto wa marehemu unaongelea watu wazima ambao wakati huu sasa wana familia zao na wana maisha yao.

Lakini niseme tu kwa kwa wale wanaostahili chochote kwa mujibu wa sheria tutaendelea ya kuonmgeza kasi ya kuhakikisha kwamba haki zao wanazipata kwa mujibu wa sheria.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na zoezi la kuorodhesha majina ya wanajeshi wote wastaafu kule Pemba. Je, nini dhamira ya zoezi hilo na ni lini utekelezaji wake utaanza? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nadhani ni swali jipya. Kuorodhesha walioathirika na vita maana kama kuorodhesha tu askari, hebu rejea nikupate vizuri.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na zoezi la kuorodhesha wanajeshi wastaafu wa vita kule Pemba, Je, ni nini dhamira ya zoezi hilo na ni lini utekelezaji wake utaanza? Ahsante.

**SPIKA:** Sawa sasa, sasa nimeelewa.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, zoezi la kuorodhesha askari walioshiriki katika vita ni zoezi la kudumu katika jeshi kuhakikisha kwamba hatupotezi kumbukumbu zao. Kwa hiyo nia ya Serikali ni hiyo kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwa na takwimu za askari ili

wanapokuwa na shida wakati wote tuweze kushughulika kwa mujibu wa sheria kwa shida zao.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Ruth Msafiri kwa sababu unakotoka kulikuwa na mapambano basi nitakupa uulize swali la mwisho.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, swali langu linahusiana na wapiganaji walioshiriki katika vita ya kumng'oa Nduli Idd Amin kule Uganda kutoka kwenye Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambao wengi wao hivi sasa wako vijijini baada ya kumaliza shughuli ile tuliyowatuma sasa wako vijijini. Wameorodheshwa kupitia Ofisi za Wakuu wa Wilaya na wanatuuliza Waheshimiwa Wabunge kila tunapopita.

Je, hivi wapiganaji wale wanastahili gani ambayo Taifa hili wanaweza wakaiangalia kwao baada ya kuwa wameshawaorodhesha katika Ofisi za Ma-*DC* wana matarajio. Sasa matarajio hayo Serikali inasema nini kuhusu matarajio haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: M**heshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na zoezi la kuorodhesha askari walioshiriki vita hii ya Idd Amin. Lakini naomba niseme kwamba kwa mujibu wa taratibu za Jeshi na sheria ya *Defence Force Act,* Askari wote walioshiriki vita amini walikwishalipwa stahili zao. Tunaendelea kuchukua tu kumbukumbu zao kwa shughuli zingine za kijeshi.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwamba askari aliyeshiriki kupigana ama ambaye hakushiriki kupigana yeyote anapojitolea kwenda katika jeshi la Kujenga Taifa kusudio lake ni kujitolea zaidi na kulinda taifa letu kwa nafasi ya kipekee zaidi. Naomba kuuliza Serikali ina utaratibu gani ambao unahakikisha pensheni za askari zinakuwa tofauti na zinalipwa kwa wakati kuliko za wafanyakazi wengine kwa nia kwamba wamejitolea nafasi zao zaidi, kutokeza vita wanakwenda mstari wa mbele kama hakuna vita wanakaa tayari kulika taifa, pensheni zao zikoje? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wafanyakazi wake na watumishi wote wa umma ambao wanafanyakazi katika nchi yetu. Kwa hiyo, kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa kuanza kuwagawa watumishi kwa makundi ya umuhimu. Watumishi wote wa umma ni muhimu kwa Serikali. (*Makofi*)

Na. 6

**Adhabu kwa Walimu wanaowanyanyasa wanafunzi**

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa kumekithiri vitendo vya walimu kuwanyanyasa wanafunzi kama ile kuwaanika juani kwa muda mrefu, kuwafanyisha kazi za majumbani na mashambani mwao jambo ambalo ni kinyume na maadili ya kazi:-

(a) Je, Serikali imemchukulia hatua gani za kinidhamu mwalimu aliyewaanika juani wanafunzi wa shule ya Msingi Wilayani Kibaha?

(b)Je, Serikali inawachukulia hatua gani za kinidhamu walimu ambao wanawatumikisha wanafunzi majumbani mwao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mwalimu wa shule ya msingi Mbwana iliyoko Wilayani Kibaha mnamo tarehe 27/01/2009 aliwapa wanafunzi saba wa darasa la saba adhabu ya kulala juani kwa muda wa nusu saa. Uongozi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa ulijadili suala hili na kuamua kumpa adhabu ya onyo karipio kali mwalimu huyo kwa kuwa lilikuwa kosa lake la kwanza.

(c) Mheshimiwa Spika, walimu ambao wanapatikana na makosa ya kuwatumikisha wanafunzi wanachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuzingatia kanuni za utumishi wa walimu na utumishi wa umma. Mpaka sasa Wizara haijapata taarifa ya walimu wanaowatumikisha wanafunzi lakini wakipatikana watachukuliwa hatua zinazostahili.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali sasa iko tayari kuboresha kanuni zake na kuongeza kifungu kitakachoweza kukatwa kwa walimu ambao wanatumikisha wanafunzi nusu ya mshahara wao au nusu ya mapato ya shamba lao ili waweze kulipwa fidia wanafunzi hao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi kwamba pale itakapobainika mwalimu ametoa adhabu au amewatumikisha wanafunzi zipo kanuni, sheria na taratibu zinazopaswa kufuatwa kumuadhibu mtumishi huyo. Kutoa adhabu Wizara au Halmashauri ya kumkataa mazao yake tutakuwa tunafanyakazi ya chombo kingine ambacho ni Mahakama na Wizara ya Elimu haina mahakimu. (*Makofi*)

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa unyanyasaji huo wa wanafunzi wakati mwingine inatokea kwa walimu wakuu kuwanyanyasa pia walimu wao wa kike pale wanawataka kimapenzi na wanapokataliwa mwalimu anapewa adhabu ikiwemo wakati mwingine kufagia darasa, kupanga kuni au wakati mwingine kutokwenda *staff room* kukutana na wenzie kubadilishana mawazo. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu hilo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikiri kwamba hadi sasa Wizara

haijapokea malalamiko ya kesi hizi ingawa kupitia Halmashauri na kwenye vyombo mbalimbali tunazisikia.

Hata hivyo naomba niseme Wizara imekuwa na mikakati mbalimbali ya kuwajengea uwezo wanafunzi wa kike ili pale wanakutana na mikasa kama hiyo, wawe na uwezo wa kukataa na kama ni kunyanyaswa iwe ni mwalimu au mtumishi mwingine waweze kutoa taarifa kwenye vyombo vinavyohusika.

Isitoshe naomba niseme kama ni ngazi ya kata yuko mratibu elimu kata, yuko mtendaji wa kata, iko ngazi ya utawala pale inaitwa *Ward C* hawa wanao uwezo kisheria kushughulikia matatizo kama haya kabla ya Wizara ya Elimu maana tuko mbali sana. Hata hivyo hili ni jambo tunahitaji sote kwa pamoja kushirikiana kulikemea maana haya ni manyanyaso mabaya sana. (*Makofi*)

Na. 7

**Ujenzi wa Chuo cha Taasisi ya Sayansi na Bahari**

**MHE. PASCHAL D. NAKEI (K.n.y. MHE. DR. HAJI MWITA HAJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa ni zaidi ya miaka mitano tangu awamu ya Bunge la Nane Chuo cha Taasisi ya Sayansi na Bahari kimekuwa kwenye ujenzi usioisha; na kwa kuwa, Mkandarasi wa Kichina aliyekuwa anajenga Chuo hicho ameacha kuendelea na kutolipwa fedha za ujenzi ambapo Serikali imeshindwa hata kudhamini mkopo wa benki kwa ujenzi huo:-

(a)Je, ni kitu gani kilichoifanya Serikali kushindwa kuendeleza ujenzi wa Chuo hicho?

(b)Je, Serikalil haioni kuwa, inajiingiza kwenye matatizo ya kukiuka mikataba yake na Mkandarasi huyo?

(c)Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Chuo hicho?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDETIA KABAKA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali imeshindwa kuendeleza mradi huo kama ilivyopangwa bali ni uhaba na mtiririko wa fedha usioridhisha. Hadi sasa kiasi kilichopatikana ni asilimia ishirini na saba nukta tano (27.5%) ya kiasi kilichohitajika mwaka 2006/2007 ili kukamilisha awamu ya kwanza.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inafanya majadiliano na Mkandarasi huyu kuhusu masharti ya mkataba ili yaendane na hali halisi ya wakati huu. Hadi sasa majadiliano yanaendelea vizuri na Serikali haijapata hasara. Mara fedha za kuendeleza mradi huu zitakapopatikana ujenzi utaendelea kwa kutumia mkataba mpya.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali ina nia thabiti ya kukamilisha ujenzi wa mradi huu. Ukamilifu wa mradi huu unategemea upatikanaji wa fedha ya kutosha katika bajeti ya maendeleo.

**MHE. NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli majibu ya Naibu Waziri ni mazuri lakini kwa upande mwingine kama alivyosema kuwa utaratibu uliopo hivi sasa wa kujenga chuo kile umekuwa wa muda mrefu na hii fedha kwa kweli haijapatikana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unatuambiaje wakati ambapo utaratibu wa mabenki wanataka kusaidia lakini Serikali yenyewe ni ngumu au tatizo kutoa huo msaada wenyewe ambao unaweza ukasaidia kulipa deni la mabenki?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA KABAKA):** Mheshimiwa Spika, msaada wa mabenki anaozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba Serikali itoe dhamana kwa ajili ya kukopa kwenye mabenki.

Hata hivyo ilikuwa tayari itoe dhamana lakini hadi sasa masharti ya dhamana ni kwamba interest itakuwa ni juu na tayari Serikali imeshadhamini miradi mingi sana.

Kwa sasa Serikali bado haijawa tayari kudhamini mradi huu na hatua ambayo sasa hivi mradi umefikia ni nzuri. Kwa hiyo, tuendelee tu kuvuta subira na tuna nia thabiti kabisa ya kuhakikisha kwamba jengo hili linakwisha na vijana wale wanahamia kutoka sehemu waliyopo na kwenda kusomea katika ile sehemu ya Buyu.

Na. 8

**Mkakati wa Kutoa Lishe na Dawa kwa Wanafunzi Waathirika**

**MHE. DORA HERIEL MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa UKIMWI umesababisha kuwepo kwa yatima wengi ambaoni waathirika na wengi wao wakiwa na wanafunzi katika shule za msingi na za sekondari, na kwa kuwa, wanafunzi hao huishi kwa kutumia dawa maalum za kuongeza maisha ARV’s ambapo watumiaji hutakiwa kupata lishe bora:-

Je, ni mikakati gani mkakati gani iliyowekwa na Serikali katika kuwahudumia watoto hawa kwa kuwapatia lishe bora na dawa pindi wakiwa shuleni?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dora Heriel Mushi Mbunge waViti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lishe shuleni ni mojawapo ya huduma zinazotolewa na mpango wa Taifa wa Afya Shuleni *(School Health Program).* Huduma hii inalenga kuwapatia wanafunzi wote chakula wakati wakiwa shuleni. Katika miaka iliyotangulia, kulikuwa na utamaduni wa jamii kuwaandalia na kuwafungashia watoto wao chakula wakienda shuleni.

Katika miaka ya 1961 hadi miaka ya 1970 Serikali ilianza kuwapatia wanafunzi wote chakula cha mshana shuleni. Huduma hii ilisitishwa baada ya kuongezeka idadi ya wanafunzi kila mwaka na kusababisha Serikali kushindwa kumudu gharama za chakula ambazo zilikuwa kubwa sana. Mwaka 2007 idadi ya wanafunzi wa shule za msingi ilikuwa 8,396,925 kutoka 6,562,772 ya mwaka 2003. *(Makofi)*

Kutokana na hali hii, Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Afya shuleni imeendelea kuhamasisha jamii na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kumpatia chakula mtoto akiwa shuleni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha mpango wa kusambaza dawa za kupunguza makali ya UKIMWI mwishoni mwa mwaka 2004. Kuanzia wakati huo hadi sasa, idadi kubwa ya Watanzania wanaoishi na virusi vya UKIMWI wameanzishiwa dawa hizo.

Hadi kufikia mwezi Januari 2009 idadi ya wagonjwa waliokuwa wakipata dawa hizo ni 211,313 ikijumuisha watoto 16,971 wa umri chini ya miaka 14 na watu wazima 194,342. Wagonjwa wote wa UKIMWI kabla ya kuanzishiwa dawa hupewa ushauri nasaha kuhusu lishe bora na UKIMWI.

Pamoja na ushauri nasaha unaotolewa kwa mgonjwa mmoja mmoja, shughuli nyingine mbalimbali zimefanyika katika jamii ili kujenga uelewa wa wananchi kuhusu UKIMWI na lishe. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

- Watoa huduma majumbani na watoa ushauri nasaha 688 katika Wilaya 39 na Mikoa 6 wamepata mafunzo kuhusu lishe kwa wagonjwa wa UKIMWI na zoezi linendelea.

- Wakufunzi 111 kutoa Vyuo vya Ualimu 37 walipewa mafunzo kuhusu UKIMWI na lishe.

- Nakala 17,000/- za Mwongozo wa Kitaifa kuhusu lishe bora kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI zimechapishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lishe kwa watoto yatima, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kupitia Mfuko wa Kimataifa wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria na

kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *PACT*, imeanzisha mpango wa kuwapatia chakula watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu.

Mpango huo unatekelezwa katika Wilaya 12 na umewafikia wtoto 17,411. Wilaya ambazo zimefikiwa na mpango hu ni pamoja na; Iramba, Geita Songea, Makete, Kahama, Bariadi, Morogoro Vijijini na Mjini, Lushoto, Handeni, Muleba na Kigoma. Lengola mpango huu ni kuwafikia watoto wote nchini. Hata hivyo watoto wanaopatiwa chakula siyo kwamba wote wana UKIMWI bali watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

**MHE. DORA HERIEL MUSHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa yatima wengi wanasoma katika shule za misingi na ni wadogo wengi wao wanaishi na bibi zao ambao ni wazee sana ambapo wale wazee hawawezi kujua hata muda wa kuwapa watoto dawa na wale watoto hawana msaada mwingine wowote pindi wanapokuwa shuleni. Je, kwa nini Serikali sasa isifanye utaratibu wa hawa watoto wapate lishe bora pale shuleni pamoja na hizi dawa za kuongeza maisha? (*Ahsante*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba suala la kuwapa watoto ambao ni waathirika wa UKIMWI ambao wako katika matibabu yule ambaye anamlea ndiyo anayepewa jukumu la kumwangalia ahakikisha kwamba dawa anameza. Kwa hiyo, itakuwa ni vigumu sana mwalimu kuanza tena kazi ya kumpa dawa yule mtoto. Mimi natoa ushauri kwamba yule atakayeona kwamba hatawezi kumpa basi atafutwe mtu mwingine ambaye anaishi naye ili aweze kusimamia suala la ugawaji wa dawa kwa sababu shule kwa kweli mwalimu hataweza kuwa na jukumu kama itabidi kwamba kwa mmoja itafikia muda wa kupewa dawa wakiwa shuleni sasa hiyo itakuwa ni kesi ambayo ni tofauti basi mwalimu anaweza akasaidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lishe, kama nilivyosema ni kwamba Serikali kupitia masharika mbalimbali wanajitahidi kutoa lishe lakini kwa sasa hivi bado inafanya mpango wa kuhakikisha kwamba mikoa mingine inafikiwa na Wilaya nyingine. Lakini nitakachosema ni kwamba sisi kama wananchi tuwe na tabia kwamba si kwa wale watoto ambao wana matatizo ya virusi ambao wanatumia dawa, lakini watoto wetu wanahitaji kupatiwa chakula wanapokuwa shuleni. Tuwepo na utaratibu katika shule zetu sisi wana jamii tuchangie basi hata chakula ambacho wakati wa mavuno tunaweza tukapeleka shuleni na hapo watoto wakaweza kupatiwa chakula kama vile uji na hii itazuia vile vile watoto wasiweze kutoka katika maeneo ya shule kwenda kutafuta chakula.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda kidogo unatupa shida. Swali linalofuata linaelekezwa Wizara hiyo hiyo linaulizwa na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya ambaye simuoni humu katika Ukumbi. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata Wizara ya Miundombinu linaulizwa na Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya.

Na. 10

**Kuboresha Kiwanja cha Ndege Cha Kimataifa cha**

**Julius Nyerere**

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ndicho Kiwanja pekee kinachotegemewa na Mashirika makubwa ya Ndege kusafirisha abiria na mizigo; na kwa kuwa, uwanja huo huonekana kwamba umezidiwa kukiwa na ndege mbili au zaidi zimetua wakati mmoja ambapo abiria wanakuwa wengi wakiwemo watalii na hupata usumbufu mkubwa sana:-

(a) Je, ni lini Serikali itachukua hatua za dharura za muda mfupi kuokoa hali hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, huu ni wakati muafaka wa kujenga kiwanja kipya kitakacholenga miaka 50 ijayo na kuboresha miundombinu itakayosaidia kuepusha kupanda kwa gharama mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, ya kwamba lipo tatizo la msongamano wa abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kiamtaifa cha Julius Nyerere hususan pale ambapo ndege mbili au zaidi zituapo kwa wakati mmoja. Kama hatua ya dharura ya kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekwishaanza kuchukua hatua za kupanua kumbi za kuondokea na kufikia abiria pamoja na kuboresha matumizi ya nafasi katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

Hivi sasa kazi ya usanifu wa upanuzi wa kumbi hizo inafanywa na Mhandisi Mshauri, Kampuni ya *Aeroproject (T) Ltd.* ya Dar es Salaam na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2009. Sambamba na hatua hiyo, Serikali inao mpango wa muda mrefu wa kuendeleza Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, ambapo kwa hivi sasa inakamilisha mazungumzo na Kampuni ya China *Sonangol International* (CSIL) kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya kupanua na kuendeleza Kiwanja hicho.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Kiwanja cha Ndege kitakidhi mahitaji ya usafiri wa anga katika miaka 50 ijayo. Maandalizi ya kukidhi mahitaji hayo yamekwishaanza kwa Serikali kupata maeneo mawili katika Mkoa wa Pwani, ambayo yanaweza kujengwa Kiwanja cha Ndege ambacho kitakidhi mahitaji ya usafiri wa anga katika miaka 50 ijayo au zaidi. Maeneo hayo yako katika Wilaya ya Bagamoyo na Mkuranga. Kwa sasa taratibu za kuyapima na kupata hati zinafanywa na Wizara yangu Miundombinu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza kuhusiana na kadhia hii.

(a)Je, ni lini au mwaka gani Serikali itakamilisha kuyapima maeneo yaliyotajwa na kupata hatimiliki hizo?

(b)Baada ya kupatikana hatimiliki hizo je, fedha za kujenga kiwanja kipya zitapatikana wapi na ujenzi utaanza lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sijui fedha zitapatikana lini nadhani si sahihi kwa sababu kama hata hati bado, labda ajibu hilo la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi ambalo tumelitoa hapa tumesema maandalizi yamekwishaanza kwa kuainisha yale maeneo katika Mkoa wa Pwani, kule Bagamoyo na Mkuranga.

Kazi tunayoifanya sasa hivi ni kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili tuweze kupata hati na baada ya hapo sasa taratibu zingine ndiyo zitafuata, lakini maandalizi kimsingi yamekwishaanza.

Na. 11

**Serikali Kujenga Barabara na Kutoa Kivuko**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali hutenga fedha na kushirikiana na wafadhili kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na barabara, madaraja, makalvati, mitaro na upatikanaji wa vivuko:-

(a)Je, ni lini barabara ya Muleba, Biharamulo, Kyaka hadi Mulushaka na ile ya Mulushaka, Benako, Ngara, Kashura hadi Maluku zitatengenezwa?

(b)Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi wa Bukoba Vijijini kupata kivuko cha kutoka Bujungo Kyenabasi ambacho kimechakaa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saverina Silavanus Mwijage, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kagoma – Muleba – Lusahunga kwa kiwango cha lami unagharimiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*. Mchakato wa kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii; baada ya Mkandarasi wa awali kusitishwa unaendelea. Wakala wa Barabara *(TANROADS)*

wameshakamilisha tathmini ya zabuni za kazi hiyo *(evaluation of tenders).* Hivi sasa Wakala wa Barabara unaendelea kufanya mawasiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kupata kibali ambacho ni lazima kitolewe na Benki hiyo kabla ya kusaini mkataba na Mkandarasi.

Kwa upande wa barabara ya Kyaba hadi Karagwe (Mulushaka), Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2008/2009 imetenga shilingi milioni 550 kwa madhumuni ya kugharimia kazi za usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Kazi ya usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni ambayo imepangwa kukamilika ndani ya miezi 6 itaanza mwezi mei 2009. Kazi za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zimepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2009/2010. Barabara ya Karagwe (Mulushaka) – Benako – Ngara inahudumiwa na wakala wa barabara Mkoa wa Kagera. Barabara hiyo ni ya tabaka la changarawe na ipo katika hali nzuri. Aidha, barabara ya kutoka Magoti Kupitia Maluku *Centre* hadi Kanyengereko inayohudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imefanyiwa matengenezo kwa kuwekwa lami sehemu ya Magoti hadi Busimbe, ambapo sehemu iliyobaki kuanzia Busimbe kuelekea Maluku imetengenezwa kwa kiwango cha Changarawe na barabara iko katika hali nzuri.

(b)Kivuko cha Kyenyabase kinachotumika sasa kilianza kufanya kazi mwaka 2004. Kivuko hicho kina uwezo wa kubeba tani 7 na kinaendeshwa na *Outboard Engine* moja yenye uwezo *HP 48.* Kivuko kwa sasa kinafanya kazi kwa kutumia kamba ya chuma kutokana *Outboard Engine* yake kuharibika mwanzoni mwa mwaka huu 2009.Wakala wa Ufundi na Umeme ulioko chini ya Wizara yangu inaifanyia ukarabati injini hiyo na kazi ya ukarabati inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei 2009. Wizara pia itatenga fedha za kununulia *outboard engine* mpya kwa ajili ya kivuko hicho katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni mazuri tu ya kuridhisha lakini waelewe kwamba hii barabara ya Muleba ni tatizo kubwa sana na mpaka sasa hivi magari hayafanyi kazi kuja Dar es Salaam. Kivuko cha Kyenyabasa mpaka sasa hivi kina matatizo makubwa, naomba Serikali iwasaidie hawa waweze kupata usafiri.

**SPIKA:** Naona ni kama ombi na taarifa tuendelee.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa ya kuuliza swali la nyongeza kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri kuhusiana na mkakati wa kujenga barabara ya Kyeka, Adomu, Mushaka Bugene baada ya shukrani hizo nilitaka nimuulize kwamba katika bajeti ya Bunge la mwaka jana bajeti ya 2008/2009 Bunge hili lilipitisha milioni 55 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kyeka mpaka Bugene na tulitegemea barabara hiyo iwe imeanza katika kipindi cha mwaka na kwa kuwa mwaka huu unakaribia mwishoni, mwaka huu wa fedha unakaribia kuisha. Je, ni kwa nini hiyo fedha ambayo imepitishwa na Bunge kwa ajili ya kujenga siyo kufanya survey, haijaanza kujenga barabara hiyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Blandes, Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru sana kwa shukrani alizozitoa kwa kutambua jitihada za Serikali zinazofanywa katika ujenzi wa barabara hapa nchini ambazo zimetajwa katika swali hili.

Lakini kuhusu swali lake la hizi fedha zilizotengwa katika kipindi kilichopita, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tumeshazungumza naye pamoja na kupewa majibu katika maeneo mbalimbali kwamba fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya kufanyia usanifu ili barabara hii iweze kuanza na kama wote tunavyofahamu kwamba ujenzi wa barabara yoyote hauwezi kuanza mpaka usanifu pamoja na upembuzi uwe umeshakamilika.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie tu kwamba kama tulivyojibu kwenye swali la msingi hapa kwamba jitihada za Serikali na dhamira ya kuijenga barabara hii ziko palepale kwahiyo namuomba tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Wilaya ya karagwe tuendelee kushirikiana pamoja na kutuunga mkono katika jitihada hizi ili kuhakikisha kwamba barabara hii tunashirikiana kuijenga na hatimaye iweze kukamilika. *(Makofi)*

Na. 12

**Kuboresha Zao la Minazi**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa, zao la minazi linategemewa sana na wananchi wa Tanzania Zanzibar na wale wanaoishi katika mikoa ya Pwani, Dar-es-Salaam, Morogoro, Mtwara na Tanga:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza hali ya soko la ndani na nje kwa zao hilo ikoje katika miaka ya hivi karibuni?

(b) Je, ni kweli kwamba, Nazi ina virutubisho vinavyosaidia kuongeza kinga ya mwili na hivyo kusaidia wagonjwa wa *UKIMWI*.

(c) Je, Serikali inatoa maelezo gani kwa wananchi juu ya zao hilo ambalo kwa sasa mbali na kushambuliwa na magonjwa pia hukatwa kwa wingi sana kutengeneza fanicha *(Samani)*?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania inayo miti ya minazi milioni 25 ambayo hutoa takribani nazi milioni 800 kwa mwaka. Nazi hizo zikisindikwa zinaweza kutoa wastani wa tani 120,000 za mafuta. Wastani wa bei ya nazi isiyopungua uzito wa nusu kilo wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani huuzwa kati ya shilingi 500 na 700 kutegemeana na hali ya soko jijini Dar-es-Salaam, bei hizi ni sawa na shilingi 1,000,000/= moja na milioni 1.4 kwa tani.

Aidha katika miezi ya kawaida bei ya nazi sokoni hushuka hadi shilingi 200 au 300 kwa nazi moja ambayo nisa wana shilingi 400,000/= hadi 600,000/= kwa tani.

Mheshimiwa Spika, katika soko la Kimataifa jijini Rotterdam Uholanzi, tani moja ya mafuta ya nazi yaliyosindikwa huuzwa kwa dola za kiamrekani 635.

(b) Mheshimiwa Spika, utafiti ulioanza kufanywa nchini Ufilipino mwanzoni mwa mwaka 2000 ulibaini na sasa umedhihirisha kwamba mbali na kusaidia kwenye mmeng'enyo wa vyakula mwilini, mafuta haya ya nazi yana asidi shahamu, yaani *fat acids*, ambazo mwili huweza kuzigeuza kuwa viini lishe aina ya *monolorin* ambazo huongeza kinga ya mwili kwa magonjwa mbalimbali yanayosababishwa na bacteria kuvu na virusi yakiwemo magonjwa ya ngozi, kisukari, na UKIMWI.

(c) Mheshimiwa Spika, minazi kama yalivyo mazao mengine ya kilimo hushambuliwa na wadudu, magonjwa na wadudu. Kwa kutambua mchango wa zao hili katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, inashauri yafuatayo katika kuendeleza zao la minazi:-

(i) Wakulima waendelee kupanda minazi asilia yaani *East African Tall*, ambayo inauwezo wa kuzaa nazi nyingi na kustahamili ukame na magonjwa mbalimbali.

(ii)Ugonjwa wa kunyong'onyea yaani *lethal disease*, uankisiwa kuwepo nchini tangu mwaka 1905. Juhudi za kitaifa na kimataifa zinaendelea kufanya uchunguzi ili kudhibiti ugonjwa huu.

(iii)Utafiti wa mbegu bora za minazi inayostahimili ukame, wadudu pamoja na kuzaa nazi nyingi, mifumo bora ya kilimo cha minazi na teknolojia za usindikaji zinaendelea katika kituo cha utafiti Mikocheni Dar-es-Salaam. Utafiti huu na huduma za ugani zitaendelea kuboreshwa ili kuliendeleza zao la minazi.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza ni kwamba, katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema chakula cha nazi au mafuta ya nazi yanasaidia kuongeza kinga mwilini. Je, sasa serikali itakuwa tayari kuwatangazia wale waathirika wa *UKIMWI* na wagonjwa wa kisukari kuwa wale nazi kwa wingi?

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba ugonjwa huu wa kunyong'onyea kwa minazi umeingia karibu miaka 104 kwa maelzo yake huko nyuma na bado haujaweza

kudhibitiwa na unaenea na wakulima wanakata tama. Je, Mheshimiwa naibu Waziri, atawaeleza nini wananchi juu ya kukata kwao tama?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kidawa kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linahusu kinga; kusema kweli mafuta yanayotokana na nazi zilizokomaa ni mazuri sana kwa afya ya binadamu. Kwasababu hata *colesteral* yake iko chini sana ambayo pengine hata ingesaidia kwenye magonjwa ya moyo kuweza kupunguza matatizo zaidi.

Lakini kama nilivyosema zile *fat acid* mwili una uwezo wa kuzibadilisha na kuzitengeneza *chemical* ambayo inaitwa *monolorin* ambayo inasaidia kinga ya mwili. Kwahiyo tunasisitiza na tunahamasisha wananchi wanendelee kutumia nazi kwasababu tunaweza tukazilima na pia tunaweza tukatumia mazao yake zaidi ili tuweze kutunza afya zetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kweli kabisa ugonjwa huu uligundulika mwaka 1905 lakini kama ilivyo katika magonjwa yanayosababishwa na virusi utafiti bado unaendelea, kama vile munavyokumbuka *UKIMWI* tangu mwaka 80 uligunduliwa lakini mpaka sasahivi wanasayansi wanaendelea kufanya utafiti. Na tuelewe kabisa kwamba wadudu wengine huwa wanabadilika kutokana na mazingira, kila unavyotafuta dawa wanabadilika wanajitengeneza sura nyingine kwahiyo inakuwa ni vigumu sana kuwapatia dawa. Lakini kwa sasa nawashauri wakulima wasikate tamaa na wafuate ushauri ufuatao:-

(i) Wapande minazi asilia yaani hii ya *East African Tall* ambayo inazalisha kwa wingi na pia inastahimili magonjwa.

(ii) Wasisafirishe miche kutoka maeneo ambayo yameathirka na ugonjwa huu kupeleka maeneo mengine.

(iii) Wachome minazi ambayo imeathirika na waweze kuikata na iuchoma kabisa.

(iv) Pia ni vema wakachanganya mazao yaani, *mixed cropping*, wawe na mazao mengi kusudi wakikosa minazi basi wanapata kwenye mazao mengine.

Na. 14

**Kuboresha Mazingira ya Biashara**

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika ripoti ya mwaka 2008 ya *Doing Business Report 2008,* Tanzania bado inaonekana kutofanya vizuri kwa kushika nafasi ya 130 kati ya nchi 175 duniani zilizofanyiwa utafiti kuhusiana na unafauu wa kufanya biashara, *easy doing business:-*

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuboresdha mazingira ya kufanya biashara ili kuweza kuwavutia wawekezaji kufanya biashara nchini?

**NAIBU WAZIRI WA VIAWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mbunge wa anayetokana na Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika katika kuandaa taarifa ya kufanya biashara, yaani *Doing Business Report,* ni pamoja na mahitaji ya kila nchi katika kuanzisha biashara, kupata leseni, kuajiri wafanyakazi, kusajili mali, kupata mikopo, kuwalinda wawekezaji, kulipa kodi, kufanya biashara nje ya mipaka ya nchi, kusimamia mikataba na kufunga biashara.

Aidha madodoso yanayotumika katika kupata taarifa zinazohusiana na mahitaji haya kwa mwaka 2008 yaliwezesha kufanyika kwa uchambuzi kuhusu matokeo ya kiuchumi na kuainisha mageuzi yalitokea wapi na kwanini. Taarifa ya mwaka 2008 ilijikita katika madhara ya ugumu wa kufanya biashara katika uwekezaji, ukuzaji wa ajira katika biashara zote na hususan fursa kwa wanawake katika ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mwaka 2008 inaonesha kuwa Tanzania iliweza kuboresha nafasi yake kutoka nafasi ya 150 mwaka 2007 hadi nafasi ya 130 mwaka 2008; ili kuboresha zaidi mazingira ya kufanya biashara nchini, Serikali inatekeleza mpango wa kurekebisha mazingira ya biashara maarufu kama *MKUMBITA* ambao unarekebisha mazingira ya kufanya biashara kwa kufanya mageuzi katika usajili wa biashara na leseni za biashara.

Mageuzi katika sheria za kazi, mageuzi katika usuluhishi wa migogoro ya biashara na mageuzi katika sheria za ardhi. Utekelezaji wa mageuzi haya unasimamiwa na Wizara husika na kwa upande wa eneo la mageuzi katika usajili wa biashara na leseni Wizara yangu inaendelea na maboresho ya sheria ya leseni za biashara Namba 25 ya Mwaka 1972, ambapo tayari sheria ya usajili wa shughuli za biashara yaani *Business Activities Registration Act Bara,* ilipitishwa na Bunge hili mwaka 2007. Kanuni za kutekeleza sheria hii zimekamilika na sheria itaanza kutekelezwa mapema katika mwaka wa fedha 2009/2010. Maandalizi muhimu ya mafunzo kwa wataalamu na maboresho ya ofisi ya usajili yanaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sheria ya usajili wa shughuli za biashara ambayo itawezesha kurahisisha uopatikanaji wa mahitaji ya kuanzisha bisahara kama vile

usajili wote kufanywa katika ofisi zilizoko katika Halmashauri na hivyo kuondoa hitaji la kufuata lesni Dar-es-Salaam kwa baadhi ya biasharra pamoja na mageuzi yanayofanywa chini ya *MKUMBITA* yataiwezesha Tanzania kuondokana na kiwango inachopewa hivi sasa katika urahisi wa kufanya biashara hapa nchini ili kiwango hiki kiweze kuwa kikubwa zaidi.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake amethibitisha mikakati na mipango mbalimbali ya mageuzi ikiwemo *MKUMBITA* na kupitishwa kwa sheria ya *Business Activities Registration Act* ya mwaka 2007 katika kusaidia kuboresha mazingira ya kufanya biashara ambayo sheria hiyo inatumika Tanzania Bara tu. Lakini kwasababu Tanzania ina sehemu mbili ina Tanzania Bara na ina Zanzibar; Je, ni kwa vipi basi na kwasababu lengo ni kuboresha biashara kwa Tanzania nzima, ni kwa vipi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inashirikishwa katika Mpango huu wa kuboresha mazingira ya biashara?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fereji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru kwa kukubaliana nasi kwamba hatua zinazofanyika zinaelekeza nchi nyetu katika hali bora zaidi. Lakini napenda nimtoe wasiwasi kuhusu kushurikishwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, shughuli za biashara haziko chini ya Muungano, lakini zipo taratibu za Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa upande wa Bara kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pale ambapo kuna jambo la msingi litakaloboresha mazingira ya kufanya biashara na mazingira ya uwekezaji kuhakikisha kwamba linalofanyika Bara na Visiwani linafanyika.

Lakini vilevile inapoonekqana kwamba utekelezaji unakuwa mzito kido, labda kunakuwa na matatizo kidogo, basi masuala haya vilevile yanapata nafasi ya kujadiliwa katika vikao vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi chini ya uenyekiti wa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo napenda nimtoe wasiwasi na kumuhakikishia kwamba haya yote yamezingatiwa na yataendelea kuzingatiwa na endapo itaonekana kuna haja ya kwenda hatua kubwa zaidi ya kufanya mambo haya yafanyike siku moja kwa wakati mmoja, basi Wizara yangu haitasita kuratibu hilo kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na biashara kwa upande wa Zanzibar.

Na. 15

**Kampuni Zinazopaki Maji Ya Kunywa Nchini**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** Aliuliza:-

Kwa kuwa, hapa nchini kumekuwa na ongezeko kubwa la kampuni zinazofunga maji ya kunywa na kuyauza kwa wananchi:-

(a) Je, kampuni hizo ni ngapi kwa majina zilizoko nchini kote?

(b) Je, maji yanayotokana na viwanda hivyo yanalingana kwa ubora wake? Na kama ziko tofauti ni zipi za kikemia kwa ujumla wake unaozingatia usalama na afya ya mtumiaji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye vipengele viwili cha (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, hapa nchini kampuni ambazo zimepewa leseni za ubora na Shirka la Viwango Tanzania kwa biashara ya kufungasha maji ya kunywa zipo 36. Kampuni hizo kwa majina na majina ya biashara ni kama ifuatavyo:-

**Dar-es-Salaam**

(i) *Aqua Cool* (Kisima);
(ii) *Super Meal (Cool Blue);*
(iii) *Bakhresa Food Products Ltd* (Uhai);
(iv) *National Manufactures and sales Agency (Sky Drops);*
(v) *Unite Manufactures & Business Ltd* (Penguin);
(vi) *A-One Products & Bottles Ltd* (Masafi);
(vii) *Cocacola Kwanza* (Dasani);
(viii) *Quingdao Industrial Investment (Snow Mountain;)*
(ix) *Sayona Drinks Ltd* (sayona);
(x) *Banit Tamim Food Products (Mtera Splash);*
(xi) *K-Cool Water Enterprises Co. Ltd (K-Cool); na*
(xii) *Great Zone Investment* (Mawenzi).

**Arusha**

*(i) Prestige Industrial Ltd* (Siringet);
*(ii) Jarry's SPA Products* (Gulfa);
*(iii) Just Water Tanzania Ltd (Just Water);*
*(iv) Halais Pro Chemie (Tefal Blue Diamond); na*
*(v) Polyfoam Ltd (Ice Berg).*

**Mwanza**

(i) *Bright Oyat Manufactures (Maweru Ice);*

(ii)*Nyanza Bottling Co. Ltd* (Dasani);
(iii)*Mona's Beverages Company* (Zam Zam); na
(iv)*Vegetable Oil Industries Ltd* (Aquava).

**Kilimanjaro**

*(i)Bonite Bottlers Ltd.* (Kilimanjaro);
*(ii)Uzima Beverages Co.* Ltd (Uzima); na
*(iii)Siha Beverages Co. Ltd* (Siha).

**Tanga**

(i)*Tanga Life Supplies (Tanga Life);*
(ii)*Usambara Spring Water* (Usambara); na
(iii)*Natural Choice Co. Ltd. (Mountain Spring).*

**Iringa**

*(i)Tanzathai – IR – Ltd.* (Africa); na
*(ii)African Benedictine of Hanga* (Chemchem).
**Morogoro**

*(i)Uluguru Fountain Ltd.* (Maji Uluguru); na
*(ii)Maji Kilombero Ltd.* (Maji Kilombero).

**Zanzibar**

(i)*Drop of Zanzibar (Drop); na*
(ii)*Zanzibar Bottlers Co. Ltd. (Kool).*

**Mtwara**

*(i)Imran Traders* (Imran).

**Tabora**

*(i)Al-Aldraus Enterprises* (Usalama).

**Dodoma**

*(i) Dodoma Innovation & Production* (A-sante)

(b)Mheshimiwa Spika, maji yanayotokana na viwanda hivyo yanakidhi ubora wa unaotakiwa kulingana na kiwango husika. Maji haya hayana tofauti kikemia wala kibaiolojia. Tofauti iliyopo ni katika vyanzo vya upataikanaji wa maji yenyewe na

utengenezwaji wake kiwandani. Serikali kwa kupitia shirika la viwango Tanzania, pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa viwango vya taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na viwango mbalimbali ambavyo shirika limetayarisha, shirika limeainisha aina mbili za viwango vya maji ya kunywa ya kufunga kwenye chupa. Viwango hivi ni kama ifuatavyo:-

*(i)TZA 573: 1999 Natural Mineral water – Specification* – Kinachohusu maji yenye asili ya Chemchemi.

*(ii) TZS 574: 2007 Packaged/Bottled Drinking Water – Specification* – Kinachohusu maji ya mito, maziwa, mabwawa na visima.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, chupa zinazotokana na maji haya zinachangia katika kuharibu mazingira. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwalazimisha wenye viwanda kuajiri ma-ajenti ambao watasafisha na kuondosha chupa hizo katika mitaa na sehemu zote zitakazokuwa takataka.

**NAIBU WAZIRI WA VIAWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni kweli kwamba matumizi ya maji haya tusipoangalia yanaweza yakachangia uharibifu wa mazingira kwasababu baada ya matumizi ya maji yale watu wanaweza wakatupa zile chupa au vile vifungashio vya kufungia maji katika maeneo mbalimbali ambayo itakuwa ni kinyume kabisa na sheria yetu ya kuhifadhi mazingira.

Kwa hiyo, nipende kusema tu kwamba Wizara yetu inajitahidi kwa kutumia shirka lake la *TIRDO* kujaribu kuhamasisha wawekezaji wa ndani kuona umuhimu wa kuweza kukusanya mabaki au chupa zile zinazotumika kwa ajili ya maji kwa ajili ya kuzitengeneza tena na kuzirudisha tena katika mfumo wa uzalishaji. Na pale kuna teknolojia na ninawakaribisha tena Waheshimiwa Wabunge wajaribu kutembelea shirika letu la *TIRDO* wataona jinsi ambavyo Wizara yangu inajitahidi kuonesha jinsi ambavyo chupa zile zinaweza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Wizara haina uwezi wa kumlazimisha kila mtanzania pale alipo aweze kuleta ile chupa, lakini tuna uwezo wa kuweka mazingira wezeshi ambayo yatamfanya mtu anayetumia maji aone kwamba ile chupa anaweza akairudisha katika mfumo wa uzalishaji na akalipwa kitu kidogo kwa maana ya fedha ambapo sasa chupa hizo zikirudishwa katika mfumo wa uzalishaji vilevile na gharama za uazalishaji maji zitapungua na zikipungua maji yatakuwa yanapatikana kwa urahisi kwa mlaji.

Kwa hiyo, nataka nitumie fursa ya Bunge hili Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania kwa kweli tuone umuhimu wa kuzirudisha chupa hizi ambazo zimetumika katika mzunguko wa uzalishaji ili kuanza kuhifadhi mazingira lakini vilevile kupata mapato yanayotokana na kukusanya chupa hizo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na kama kawaida ni matangazo. Ila kwenye jibu la Mheshimiwa naibu Waziri wa Viwanda, maneno haya kitu kidogo yana maana kidogo katika jamii ambayo ukisema unamlipa kitu kidogo maana yake si nzuri sana. *(kicheko).*

Basi matangazo tunaanza na wageni. Waheshimiwa Wabunge leo tena tumefikiwa na wageni kutoka nchi jirani na kwa leo tunao Waheshimiwa Wabunge, kutoka Bunge la Jamhuri ya Namibia. Hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali na pia Wajumbe wa Kamati ya Uchumi wakifuatana na Afisa mmoja; kwasababu ya tatizo la lugha, itabidi niongee kingereza sasa kuwatambulisha.

*Members of The House, it's a pleasure once again to receive distinguished visitors from a Sister Republic of Namibia of which, we have extremely close ties. These are Honourable Members of the House of Namibia, from the Committee of Public Accounts and also Economy, accompanied by an Official of the Parliament, I will mention their names. Our distinguished guests when I mention your please stand up so the house can acknowledge you; I start with the Chair of the Committee, The Honourable Sebastian Ignatius Gobs. The Honourable Rosalia Mwadina Sibia, the Honourable Fredda Mwadina Siwombe.* Hawa wenzetu jinsia wanaangalia sana naona. *The Honourable Johannes Kamati Nakwafila, the Honourable Theo Vivian Diegard accompanied by Miss Dorothea Francmen; may be she is on the house keeping duties for the delegation. (Makofi).*

*We are extremely pleased to have you with us colleagues from Namibia. It is always pleasure to have people from the region visiting each other. Welcome to Dodoma and I am sure my stafsf are taking very good care of you. Thank you very much and our best regards when you go back.*

Wageni wengine ni watayarishaji 64 wa vipindi vya elimu kwa umma kupitia *TBC* wakiambatana na viongozi ambao ni bwana Oni Sigala, Mwenyekiti wa Mpango huo. Profesa Herman mwansoko, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Utamaduni; Bwana Tido Mhando, Mkurugenzi Mkuu wa *TBC,* Dokta Anna Kishe, Katibu Mtendaji wa *BAKITA.* Bi Edna Rajabu, Mkuu wa Mipango *TBC,* na Bi Irene Chidosa, Katibu wa Mkutano huo. Baadhi yao nadhani wametoka wameshaanza kuendelea na shughuli nyingine. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo la wageni, sasa lipo tangazo la kikao. Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali *PAC,* anawaomba wajumbe wote wa *PAC* wakutane leo katika ukumbi namba 231, ghorofa ya pili Jengo la Utawala.

Kwa hiyo, wajumbe wa Kamati ya hesabu za Serikali, mara baada ya matangazo haya wakutane katika ukumbi namba 231, Jengo la Utawala. Huo ndio mwisho wa matangazo ya kawaida.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, ni kawaida ya Bunge letu kabla hatujaendelea sana na nina hakika kabla hata ya kuanza tunakuwa na *Briefing* ili kuelezana kwa undani mambo tutakayoyashughulikia. Kwa bahati mbaya safari hii Spika na Naibu Spika, kwa kuzingatia majukumu ya uwakilishi wetu katika taasisi za nje, tumekuwa safarini.

Mimi nimerudi jana usiku kutoka Bermuda na Naibu Spika, alikwenda kwenye uchaguzi wa kumchagua Katibu wa *SADC Parliamentary Forum,* yeye katika nafasi yake kama Makamu Mwenyekiti wa *SADC Parliamentary Forum* na mimi nilikuwa Bermuda kuwawakilisha kama Rais wa Chama Cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola. *(Makofi).*

Kwahiyo haikuwezekana kufanya *briefing* na nilimtaarifu Mheshimiwa Waziri Mkuu hivyo.

Kwa hiyo, tutakuwa na *briefing* leo asubuhi saa 5.30. Saa 5.30 asubuhi ukumbi wa Msekwa ndio *briefing* na baada ya hapo shughuli nyingine zitaendelea.

Kutokana na hali hiyo basi nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 4.42 Asubuhi, Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu wa Mwaka 2009
### *(The Human DNA Bill, 2009)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ajenda yetu leo jioni tutaanza na Muswada wa Sheria ya DNA; na kama tulivyoongozwa na Katibu wa Bunge, basi sasa tutamwita mtoa mada, ambaye ni Waziri mwenye dhamana ya afya, aweze kutuletea Muswada huo. Karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Kusimamia Teknolojia ya DNA ya Binadamu ya Mwaka 2008 *(The Human DNA Regulation Act, 2008),* kama ulivyopangwa katika shughuli za leo, pamoja na jedwali la marekebisho kama lilivyoambatishwa, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa hoja yangu, awali ya yote, kwa majonzi na masikitiko makubwa na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Rungwe Magharibi, pamoja na wafanyakazi wote wa Sekta ya Afya, naomba kutoa pole kwa wafiwa; Wananchi wa Jimbo la Busanda, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wananchi na Watanzania kwa ujumla, kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Jimbo la Busanda na Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, Hayati Faustine Kabuzi Rwilomba. Mwenyezi Mungu, mwenye rehema nyingi, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa rambirambi hizo, sasa ninayo heshima kubwa, kusimama mbele yenu ili niweze kuwasilisha hoja ya Muswada wa Sheria ya Kusimamia Matumizi ya Teknolojia ya DNA ya Binadamu. Kwa mara nyingine tena, kabla sijawasilisha hoja yangu, naomba nichukue fursa hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kuupitia Muswada huu Dar es Salaam na hapa Dodoma, chini ya Uenyekiti wa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Jimbo la Muyuni Zanzibar. Kamati hii iliweza kuuchambua kwa kina Muswada ulioko mbele yenu na kutoa michango na maelekezo ambayo yameniwezesha kuwasilisha Muswada huu hapa Bungeni. Jedwali la Mabadiliko kama lilivyosambazwa ni matokeo ya uchambuzi wa kina, michango na ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa kuchangia Muswada katika ngazi ya Kamati. Nawashukuru sana.

Vilevile sina budi kutoa shukrani zangu kwa Tume ya Kurekebisha Sheria, ambayo kwa kutumia mada ya dhana *(Concept Paper)*, iliyoandaliwa na Wizara, iliweza kutembelea Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Ruvuma, Mbeya, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa na Morogoro, ambapo waliweza kupata maoni mbalimbali ya wadau, ambayo ndiyo msingi wa Muswada ulio mbele yenu. Naishukuru pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara ya Mwandishi Mkuu wa Serikali, katika hatua zote za maandalizi na hatimaye kukamilisha Muswada huu. Aidha, shukrani za kipekee ziwaendee wadau wote, ambao kwa namna moja au nyingine, walichangia kutoa maoni katika hatua za awali za maandalizi na hatimaye katika kuukamilisha Muswada huu. Naomba niwatambue wadau ambao walishiriki kutoa maoni yao wakati Muswada huu ulipowasilishwa mbele ya Kamati ya Huduma za Jamii Jijini Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

*The Muhimbili University of Health and Allied Sciences, Youth Action Volunteers, Herbert Kairuki Memorial University, National Organization for Legal Assistance, The Tanganyika Law Society, The University of Dar es Salaam, The Ifakara Health Institute,* Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na *Mental Health Association of Tanzania*. Wadau wote hawa nawashukuru kwa michango yao, kwani imesaidia sana kuuboresha Muswada ulio mbele yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitisha sheria hii ni moja ya utekelezaji na maagizo ya Serikali, pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ujumla. Lengo kuu likiwa ni kuwalinda wananchi wote, yaani watumiaji na wale wanaoweza kuathirika na matokeo ya uchunguzi wa teknolojia ya DNA ya Binadamu. Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa sheria inayokusudia kuweka utaratibu wa

kisheria utakaosimamia, kuendeleza na kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kutumia teknolojia ya DNA ya binadamu nchini na kutoa adhabu kwa wale watakaokiuka sheria ya matumizi ya teknolojia hii.

Kabla sijaanza kutoa maelezo hayo ni vyema nikaeleza historia fupi ya teknolojia ya DNA ya binadamu nchini, chimbuko na madhumuni ya Muswada, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu na matokeo yanayotarajiwa baada ya kupitishwa kwa Muswada huu na kuwa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Teknolojia ya DNA ya binadamu imekuwa inatumika hapa nchini bila ya kuwepo kwa sheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi yake. Teknolojia hii imekuwa inatumika na wadau wa aina mbalimbali; wakiwemo watu binafsi na Asasi za Kiraia katika upelelezi, tiba, kinga na tafiti. Kutokana na kutokuwepo kwa sheria imekuwa ni vigumu kuratibu, kusimamia na kudhibiti matumizi ya DNA ya binadamu, ambayo yanaweza yakatumiwa na watu wasio waaminifu, kwa manufaa yao bila ridhaa ya wenye sampuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, DNA ni kifupi cha neno *Deoxy-ribonucleic Acid*. Hizi ni chembechembe asili za urithi au viinitete, ambavyo hupatikana katika kila kiumbe kilicho hai. Uvumbuzi na matumizi ya teknolojia ya DNA ya binadamu (chembechembe asili za urithi au vinasaba), umeonekana kuwa na faida kubwa duniani kote hususan katika kinga, tafiti na tiba; hivyo, kuboresha utoaji wa huduma za afya. Kwa mfano, kutambua magonjwa ya urithi kabla na baada ya mtoto kuzaliwa, kuchukua tahadhari na kutengeneza tiba ya magonjwa hayo, kuangalia ubora na madhara ya dawa na viini lishe mwilini, matibabu ya kutumia viungo na kutambua jinsia tawala kwenye watoto wanaozaliwa na jinsia mbili.

Pamoja na kwamba, teknolojia hii imeleta maendeleo kwenye nyanja za tiba na utafiti, nchi nyingi duniani pia hutumia matokeo ya DNA ya binadamu katika kutoa haki za kisheria zinazohusiana na makosa ya jinai na migogoro ya kijamii. Kwa mfano, Polisi, Wapelelezi, Wanasheria na Mahakama, zinatumia matokeo ya uchunguzi wa DNA ya binadamu kwa kuwatafuta, kuwakamata, kuwashtaki, kuwahukumu na hata kuwaachia huru, wale waliohukumiwa kimakosa. Matokeo ya uchunguzi wa DNA ya binadamu pia huthibitisha uhalali wa mtoto kwa wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo ya awali, umuhimu wa kuwa na sheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya teknolojia ya DNA ya binadamu imetokana na sababu zifuatazo:-

(i) Matumizi ya teknolojia ya DNA ya Binadamu yamepanuka kwa sekta binafsi; hivyo, kuhitaji sheria itakayosimamia, kuratibu na kudhibiti utoaji wa huduma hii.

(ii) Sampuli za DNA ya Binadamu hubeba taarifa binafsi za siri za chembe chembe asili za urithi au vinasaba vya kila kiumbe hai akiwemo Binadamu, ambazo hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Hivyo, kuhitajika usimamizi na udhibiti wa

ukusanyaji, uhifadhi, ufungashaji, usafirishaji, upokeaji, uchunguzaji, utunzaji, uchambuzi, utoaji wa majibu na uteketezaji wa sampuli za DNA ya Binadamu unaozingatia maadili ya kitaalamu na miongozo ya kisheria. Hii itaweza kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi mabaya ya huduma hii.

(iii) Kuwepo kwa sheria hii kutasaidia kuondoa upungufu uliopo na kuweka mwongozo na utaratibu mzuri wa kuratibu, kusimamia na kudhibiti matumizi ya teknolojia ya DNA ya Binadamu hapa nchini. Aidha, kuwepo kwa sheria kutahakikisha haki za kisheria, usiri, maadili na haki za binadamu zinalindwa.

(iv) Malalamiko ya wananchi juu ya kuibiwa na/au kubadilishiwa watoto au ndugu zao, kufungwa bila ya kuhusika katika mashtaka ya makosa ya jinai.

(v) Malalamiko ya washtakiwa na/au wafungwa kuchukuliwa sampuli zinazodhalilisha utu wao na kukiuka haki za Binadamu. Kwa mfano, kuna wakati washtakiwa wamekuwa wakilazimishwa kutoa mbegu za kiume (*sperms*), kwa ajili ya DNA ya Binadamu; wakati jasho, mate au kipande cha nguo ya mshtakiwa, kinatosha kuchukiliwa kama sampuli na kupata majibu juu ya kuhusika au kutohusika kwao katika shtaka husika.

(vi) Kutatua matatizo ya uhamiaji na utambuzi wa asili ya watu.

(vii) Kuweza kutambua wahanga wa majanga mbalimbali; kwa mfano, matukio ambayo hayakuweza kupatiwa ufumbuzi wa kutambua waathirika wa majanga kama ajali ya moto ya Shule ya Shauritanga mwaka 1994, ajali ya MV Bukoba tarehe 21 Mei, 1996 na ajali ya Treni Dodoma Juni, 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko yanayotokea katika Sekta ya Afya hususan katika matumizi ya teknolojia mbalimbali ikiwemo ya DNA ya Binadamu katika nyanja za kinga na tiba, imekuwa ni muhimu kuwa na Sheria ya Kusimamia Matumizi ya DNA ya Binadamu, kwa madhumuni ya kuboresha huduma hii katika jamii na kuilinda na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi holela ya teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu ni kuwasilisha mapendekezo ya nia ya Serikali ya kutunga Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Matumizi ya Teknolojia ya DNA ya Binadamu ili kulinda afya za wananchi, usalama wa taifa na upatikanaji wa haki za kisheria, kulinda usiri, maadili na haki za binadamu, pamoja na tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika kuuandaa Muswada huu ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Sera ya Afya ya Mwaka 1990 kama ilivyorejewa mwaka 2007, ambayo inaelekeza kuwepo kwa mfumo wa kisheria wa kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma mbalimbali za afya, ikiwemo ya matumizi ya teknolojia ya DNA ya Binadamu.

(ii) Kuainisha aina ya sampuli zinazoweza kukusanywa kama vile mate, nywele zenye shina, mkojo, kinyesi, damu, jasho, ngozi, mifupa, mbegu za kiume, mpanguso wa sehemu za siri za kike *(vaginal swab)* na vifaa au vitu visadikiwavyo kuwa na mabaki ya sampuli zilizotajwa hapo juu.

(iii) Itaweka utaratibu wa ukusanyaji, ufungashaji, usafirishaji, upokeaji, utunzaji, utoaji wa majibu na uteketezwaji wa sampuli za DNA ya Binadamu ikijumuisha za makosa ya jinai.

(iv) Kuweka utaratibu wa kuzingatia katika kuondoa utata kwa wazazi pale wanaposhindwa kuafikiana juu ya upimaji wa DNA ya Binadamu ili kuthibitisha uhalali wa mtoto.

(v) Kuweka utaratibu wa kufuata katika kufanya tafiti mbalimbali za magonjwa, dawa na lishe kwa kutumia DNA ya Binadamu.

(vi) Kuainisha haki za mtu anayetoa sampuli za DNA ya Binadamu.

(vii) Kuweka utaratibu wa utoaji wa fidia kwa mtu aliyeathirika na ukiukwaji wa haki zake chini ya sheria itakayotungwa.

(viii) Kuainisha maafisa waliopewa idhini ya kukusanya, kuchambua na kudhibiti sampuli za DNA ya Binadamu na kufanya ukaguzi wa maabara za DNA ya Binadamu.

(ix) Kuweka utaratibu wa utunzaji na utoaji wa siri za matokeo ya sampuli za DNA ya Binadamu.

(x) Kuweka mipaka ya matumizi ya sampuli za DNA ya Binadamu.

(xi) Kuondoa hiari katika uchukuaji wa sampuli za aina hii katika makosa ya jinai na maafa.

(xii) Sheria itaainisha makosa na adhabu zake kwa maabara, taasisi, asasi na watu watakaokiuka utaratibu mzima wa matumizi na utoaji wa siri wa majibu ya DNA ya Binadamu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutungwa kwa sheria hii, kutaleta mafanikio mengi yakiwemo kulinda afya, usiri wa taarifa binafsi za wananchi na maslahi ya taifa kwa ujumla. Inatarajiwa kwamba, baada ya sheria hii kupita na kutekelezwa kikamilifu, matokeo yafuatayo yatapatikana:-

(i) Itaongeza ushirikishwaji wa sekta mbalimbali katika kulinda mchakato mzima wa teknolojia hii ya DNA ya Binadamu.

(ii) Itasimamia na kudhibiti matumizi yasiyo rasmi ya sampuli za DNA ya Binadamu.

(iii) Udhibiti wa sekta binafsi ya afya juu ya matumizi sahihi ya teknolojia hii bila kuathiri haki za wananchi na udhibiti wa maabara, taasisi, asasi zinazotoa na zitakazotoa huduma ya teknolojia ya DNA ya Binadamu kwa wananchi.

(iv) Matokeo ya uchunguzi wa DNA ya Binadamu yatatumika katika kutoa haki kisheria kwenye makosa ya jinai na madai ya watoto, utafiti wa magonjwa mbalimbali hatimaye kupata kinga au tiba mbadala.

(v) Kuanzishwa kwa *National DNA Database (NDNADB)* ya binadamu, ambayo pamoja na mambo mengine, itaisaidia nchi katika kubaini wahamiaji haramu, wahalifu sugu, raia wanapofariki katika maafa, kuwatambua raia wake waliopotea wakiwa hai, wafu au katika utata.

(vi) Itaainisha utaratibu wa utafiti wa kutumia sampuli za DNA ya Binadamu kuhusiana na masuala ya kimaadili na kiutamaduni.

(vii) Sheria hii itakapotungwa itasababisha sheria mbalimbali zilizopo kurekebishwa. Sheria zitakazoguswa ni kama vile *The Affiliation Act, Cap. 278 R.E. 2002; The Law of Marriage Act, Cap. 29 R.E. 2002; The National Institute of Medical Research Act, Cap. 59 R.E. 2002; The Criminal Procedure Act, Cap. 20 R.E. 2002, The Children and Young Persons Act Cap. 13 R.E. 2002; The Evidence Act, Cap. 6 R.E. 2002; The Mutual Assistance in Criminal Matters Act, Cap. 254 R.E. 2002; The Notary Public and Commissioner for Oaths Act, Cap. 12 R.E. 2002; The Immigration Act, Cap. 54 R.E 2002 na The Birth and Death Registration Act, Cap. 108 R.E 2002.*

Sheria hizi zitarekebishwa ili kuweka vipengele ambavyo vitatambua matumizi ya teknolojia ya DNA ya Binadamu, kulingana na mahitaji ya sheria husika; mfano, tafiti mbalimbali, kutambua uhalali wa mzazi kwa mtoto, kutumika kama ushahidi katika kesi mbalimbali, kutambua mabaki ya watu waliokufa katika mazingira ya utatanishi, uhamiaji, uraia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi muhimu wa mambo yaliyozingatiwa, naomba kutoa muhtasari wa yale yaliyomo katika Muswada huu, ambao umegawanyika katika sehemu kumi na moja kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya utangulizi au maelezo ya awali ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa na matumizi ya sheria hii, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria na tafsiri ya maneno na misamiati mbalimbali iliyotumika katika Muswada huu.

Shemu ya pili, inahusu mambo ya utawala ambapo imemtamka Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa ndiye atakayekuwa Msimamizi na Mdhibiti wa Sheria hii. Aidha, sehemu hii imeainisha madaraka na kazi zake chini ya sheria husika. Pia inatamka kuanzishwa

kwa Kamati ya Kitaalamu itakayokuwa inamshauri Mdhibiti. Vilevile, inatamka juu ya kuteuliwa kwa maafisa walioidhiniwa, mamlaka na kazi zao chini ya sheria hii.

Sehemu ya tatu, inahusu utaratibu wa uanzishaji wa maabara zitakazokuwa na kibali cha kuendesha, utumaji wa maombi na utoaji wa leseni kwa ajili ya maabara zinazotaka kuendesha kazi zake kwa kutumia DNA ya Binadamu. Aidha, sheria inaainisha muda wa vibali husika na uwezo wa kubatilishwa mtu anapokiuka masharti ya sheria hii.

Sehemu ya nne, inahusu ukusanyaji na uchambuzi wa sampuli za DNA ya Binadamu. Aidha, sehemu hii inazuia ukusanyaji na uchambuzi wa sampuli hizo pasipo kibali cha maandishi cha Mdhibiti, pamoja na yule anayetolewa sampuli ya DNA. Pia haki za mwenye sampuli zimeainishwa katika kifungu cha 27 kinachosomwa pamoja na kifungu cha 28 cha Muswada huu.

Sehemu ya tano, inahusu vifungu vinavyozuia utafiti wowote ule bila kibali cha maandishi toka kwa Mdhibiti. Inazuia pia ukusanyaji kwa njia ya udanganyifu au kwa kutumia fedha au nguvu (*coercion and undue influence).*

Sehemu ya sita, inahusu ukusanyaji wa sampuli kutoka kwa akina mama wajawazito na mimba changa (*foetus and extra corporeal embryo)* na taratibu za kufuata wakati wa ukusanyaji wa sampuli hizo.

Sehemu ya saba, inahusu ukusanyaji wa sampuli kutoka kwa watoto na watu wasio na nguvu za kisheria kufanya maamuzi yanayohusu hatima ya maisha yao mbele ya Afisa Ustawi wa Jamii ikiwa tayari amepata kibali kutoka kwa mzazi au mlezi wake.

Sehemu ya nane, inahusu zuio na utaratibu wa kutoa taarifa za uchambuzi wa DNA ya Binadamu. Aidha, sehemu hii inatoa utaratibu wa kuharibu sampuli hizo za DNA baada ya uchambuzi na kutoa majibu.

Sehemu ya tisa, inahusu masuala ya vyanzo vya fedha zitakazotumika katika utekelezaji wa sheria hii na kwamba, ukaguzi wa fedha utafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali.

Sehemu ya kumi, inaainisha makosa na adhabu pale mtu anapokiuka masharti ya Sheria hii.

Sehemu ya kumi na moja, inahusu mambo ya jumla ikihusisha kuweka kinga kwa maafisa watakaofanya makosa kwa nia njema wakati wanapotekeleza sheria hii. Aidha, inampa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa sheria hii. Sehemu hii vilevile inatoa haki kwa raia kushtaki kwa ajili ya fidia pale haki zake chini ya sheria hii zitakapokiukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo haya, kwa heshima kubwa, naomba Waheshimiwa Wabunge, wajadili Muswada ulio mbele yao na kuridhia na

hatimaye kuupitisha na kuwa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Matumizi ya Teknolojia ya DNA ya Binadamu, 2008 *(The Human DNA Regulation Act, 2008).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitamwita Msemaji wa Kamati ili aweze kutoa maoni ya Kamati. Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati za Huduma ya Jamii.

**MHE. OMARI S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Kabla ya kutoa taarifa hii, naomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kutoa salamu za pole na rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Busanda, Geita, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, ambaye alikuwa Mjumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa limempoteza Kiongozi shupavu, mcheshi na jasiri, aliyekuwa mstari wa mbele katika kutetea maslahi ya Taifa letu. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii, kumkaribisha Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Mwenyekiti kuwa Mjumbe wa Kamati hii. Tunamkaribisha kwenye Kamati yetu na kumhakikishia ushirikiano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, sasa naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, yanayohusu Muswada wa Vinasaba vya Binadamu, 2008 *(The Human DNA Regulation Bill, 2008).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Duniani kote, kumekuwa na mabadiliko mengi katika Sekta mbalimbali ikiwemo ya Afya. Mabadiliko hayo yanagusa sana maisha ya jamii, hasa katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia. Hapa Tanzania, wadau mbalimbali, asasi za kiraia na watu binafsi, wamekuwa wakitumia teknolojia ya vinasaba vya Binadamu (DNA) katika shughuli za tiba, utafiti, upelelezi na kinga, kwa muda mrefu bila udhibiti wa kisheria. Hivyo, kukosekana kwa sheria madhubuti ya kuisimamia teknolojia hii, kunaweza kuleta athari kubwa kwa Binadamu kwa sababu zifuatazo:-

- Sampuli za DNA ya Binadamu hubeba taarifa binafsi za siri za chembe chembe asili za urithi au viini tete, ambazo hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Hivyo ni

muhimu kuzingatia maadili ya kitaalam na mwongozo wa kisheria ili kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi mabaya ya huduma hii.

- Kukosekana kwa Sheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya Teknolojia ya DNA ya Binadamu kunaathiri sana haki za watu, usiri, maadili na utu wa Binadamu.

- Kukosekana kwa Sheria hii pia kumeleta malalamiko kutoka kwa wananchi, juu ya mazingira ya kuibiwa watoto, kubadilishwa kwa watoto na kusingiziana juu ya uhalali wa wazazi wa watoto na kadhalika.

- Vilevile kumekuwepo na malalamiko ya washtakiwa au wafungwa kuchukuliwa sampuli zinazodhalilisha utu wao na kukiukwa kwa haki za Binadamu. Mfano, kutoa manii *(sperms*), kwa ajili ya vipimo vya DNA ya Binadamu wakati jasho, mate au kipande cha nguo ya mshtakiwa kinatosha kuchukuliwa kama sampuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo hayo mafupi, Kamati ya Huduma za Jamii, inaunga mkono Mswada huu na kwamba, tunaridhia kuwa mambo muhimu yamezingatiwa katika Muswada huu ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

- Utaratibu wa utoaji wa fidia kwa mtu atakayeathirika na ukiukwaji wa haki zake chini ya Muswada wa Sheria inayopendekezwa.
- Uwekaji wa utaratibu wa utunzaji na utoaji wa siri za matokeo ya sampuli za DNA ya Binadamu yamezingatiwa.

- Kuwepo kwa vifungu vya mipaka ya matumizi ya sampuli za DNA ya Binadamu.

- Muswada pia umeainisha maafisa watakaokusanya, kuchambua na kudhibiti sampuli za DNA ya Binadamu na kufanya ukaguzi wa Maabara ya DNA ya Binadamu.

- Muswada umeainisha makosa na adhabu kwa Maabara, Taasisi na watu watakaokiuka utaratibu mzima wa matumizi ya utoaji wa siri wa majibu ya DNA ya Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaafiki matokeo ya Sheria hii yatakuwa pamoja na kuanzishwa kwa *National DNA Database* (NDNADB) ya Binadamu, ambayo itasaidia nchi kubaini wahamiaji haramu, wahalifu sugu na pia raia wanapofariki katika maafa na/au kuwatambua raia wake waliopotea wakiwa hai, wafu au katika hali ya utata.

Kamati inaishauri Serikali kuwa ili Sheria hii iweze kufanya kazi zake vizuri kuna haja ya kurekebisha Sheria muhimu tisa kama ifutavyo: *The Affiliation Act, Cap. 278 R.E. 2002; The Law of Marriage Act, Cap. 29 R.E. 2002; The National Institute of Medical Research Act, Cap.59 R.E. 2002; The Criminal Procedure Act Cap. 20 R.E. 2002; The Children and Young Persons Act, Cap.13 R.E. 2002; The Evidence Act Cap. 6 R.E. 2002; The Mutual Assistance in Criminal Matters Act, Cap. 254 R.E. 2002; The*

*Notary Public and Commissioner for Oaths Act, Cap.12 R.E. 2002; na The Adoption Act, Cap 335 R.E. 2002.*

Marekebisho ya Sheria hizi, yazingatie kuweka vipengele ambavyo vitatambua vipimo vya DNA ya Binadamu kulingana na hitaji la Sheria husika; mfano, kutambua mabaki ya watu waliokufa katika mazingira tata na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imekutana mara tatu kuujadili Muswada wa Sheria wa Vinasaba vya Binadamu, 2008. Vikao viwili vilifanyika Ofisi ya Bunge Dar es Salaam na kikao kimoja katika Ofisi ya Bunge Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha kwanza, Kamati ilipata maelezo ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kuhusu madhumuni ya Muswada, pamoja na jedwali la marekebisho ya makosa ya uchapaji. Aidha, wadau mbalimbali walishirikishwa ikiwa ni pamoja na Kituo cha Haki za Binadamu; Chuo Kikuu Muhimbili; *Youth Action Volunteer; National Organisation for Legal Assistance (nola*); Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Herbert Kairuki; Chama cha Wagojwa wa Akili; *Tanganyika Law Society;* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; *Ifakara Health Institute;* na Wizara ya Mambo ya Ndani (Jeshi la Polisi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawashukuru sana Wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni, ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii katika kuishauri Serikali ili iyazingatie katika Muswada wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha pili, Kamati ilipitia sehemu, ibara na vifungu vya Muswada na kuishauri Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu, kurekebisha ibara, maneno, makosa ya uchapaji na sentensi ili yaendane na lugha ya kisheria. Baadhi ya marekebisho yaliyoainishwa na Kamati ni pamoja na:-

(i) Kifungu cha 29 cha Muswada; Kamati inashauri kuwepo kwa nyongeza inayoonesha uhusiano kati ya *Human DNA* na *Non-Human DNA.*

(ii) Katika kifungu cha 38(3) cha Muswada, Kamati inashauri kuwepo na nyongeza “f” ambayo itazungumzia utaratibu wa *intellectual property rights*, inayopatikana kutokana na tafiti za ugunduzi wa Vinasaba vya Binadamu.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa Kifungu cha 46(1) cha Muswada kifanyiwe marekebisho ili kiweze kuleta maana iliyokusudiwa kwa mujibu wa Muswada.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 15 cha Muswada, Kamati inashauri kuwa, kazi za *Human DNA Laboratory* katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ziainishwe ili kusaidia kutenganisha kazi za maabara ya Mkemia Mkuu na maabara teule *(designated laboratory*).

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kifungu cha 18(3) cha Muswada hakitoi fursa kwa mwombaji kuomba upya au msimamizi kupitia upya maamuzi yake, pamoja na kutoa haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa msimamizi; Kamati inashauri kuwa kipengele hiki kifanyiwe marekebisho.

(vi) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kifungu cha 39 cha Muswada hakioneshi masharti na jinsi ya kufanya maamuzi, kwa niaba ya makundi ya watu ambao kwa jinsi walivyo, hawawezi kufanya maamuzi yao wenyewe; Kamati inatoa angalizo kuwa, Sheria iweke masharti na jinsi ya wazazi wao kufanya maamuzi kwa niaba ya makundi ya watu hawa.

(vii) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 29(2) cha Muswada, Kamati inashauri kuzingatia kuonesha uhusiano kati ya Vinasaba vya Binadamu na Vinasaba visivyokuwa vya Binadamu *(Non Human DNA)*.

(viii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuainishwa kwa maelezo ya viini vya DNA na RNA katika Muswada huu ili kuweka wazi uhusiano kati ya DNA na RNA.

(ix) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 30(3) cha Muswada, Kamati inashauri kuwa uchukuaji wa sampuli za DNA ya Binadamu, uzingatie zaidi utaalam badala ya jinsia

(x) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 67(2) cha Muswada adhabu iliyotolewa kwa mtu anayetoa taarifa kuhusu vinasaba vya Binadamu ni ndogo ukilinganisha na uzito wa kosa hilo, Kamati inashauri kuwa, adhabu hiyo iwe si chini ya shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka mitatu au adhabu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa angalizo kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inahitaji kuwa makini na tunashauri kuwa, uandishi wa Miswada ya Sheria ufanywe na watu makini na wenye uzoefu, kwa sababu, Kamati imetumia muda mrefu katika kuelekeza makosa yanayotokana na uchapaji na mengine ya uandishi. Mfano kwenye vifungu vifuatavyo ambavyo tumeomba virekebishwe ni:-

Sehemu ya I

Kifungu cha 3.

Sehemu ya II

Kifungu cha 5 (1) d, 5(1) f, 5 (1) j,
Kifungu cha 6 (1) g, 6(1) h,
Kifungu cha 8 (1), 8 (1) a, 8 (2),
Kifungu cha 9 (d), 9 (e),
Kifungu cha 11,
Kifungu cha 12 (2).

Sehemu ya III

Kifungu cha 15 (2),
Kifungu cha 17 (3) c,
Kifungu cha 17 (3) e,
Kifungu cha 21 (4).

Sehemu ya IV
Kifungu cha 25 (2) c,
Kifungu cha 28 (2) j,
Kifungu cha 30 (3),
Kifungu cha 31 (2),
Kifungu cha 32,
Kifungu cha 34 (5).

Sehemu ya V
Marekebisho ya Kichwa cha sehemu tano.
Kifungu cha 38 (1), (2).

Sehemu ya VI
Kifungu cha 45.

Sehemu ya VII
Kifungu cha 48 (1) b, c, d, e.

Sehemu ya VIII
Marekebisho ya kichwa cha sehemu ya nane pamoja na *Margin*.
Kifungu cha 58 (1) b, na 58 (4),
Kifungu cha 59 *Margin*,
Kifungu cha 61 (b),
Kifungu cha 62,
Kifungu cha 63 (2),
Kifungu cha 65 (1).

Sehemu ya X
Kifungu cha 67 (1) c, e, 67 (2), 67 (3) e, 67 (3) h, 67 (4) na 69.

Sehemu ya XI
Kifungu cha 70 (1) e na 75 (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha tatu, Kamati ilikutana na Serikali kuona kama marekebisho na sehemu za nyongeza zilizokubaliwa kuwa zitaonekana katika Jedwali la tatu, ambalo Mheshimiwa Waziri atalileta mbele ya Bunge lako Tukufu na kama ambavyo tayari imekwishagawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati yangu inamshukuru Waziri wa Afya, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, pamoja na Wataalamu wao wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Blandina S. J.

Nyoni, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati inaufikiria Muswada wa DNA ya Binadamu, 2008. Aidha, Kamati inawashukuru Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ufafanuzi walioutoa wakati Kamati inaufikiria Muswada huu. Vile vile Kamati inawapongeza wadau wote, walioitikia wito wa kushiriki katika vikao vya mashauriano na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu. Kamati inathamini michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa kutoa maoni yao katika kuuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Haji Mwita Haji - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhil, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Dkt. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Dkt. Luka Jelas Siyame, Mheshimiwa Fatma Abdullah Tamim, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale, pamoja na mimi Omari S. Kwaangw'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Kamati hii, Ndugu Hosiana John, kwa kuratibu vikao vya Kamati hadi maoni haya kutoka katika muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kushauri Muswada upite katika hatua zake zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikia Mheshimiwa Omari Kweaangw', akitoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Bunge ya Huduma za Jamii, sasa ninaomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hiyo. Namwona Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali.

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama tena mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya DNA ya Binadamu wa Mwaka 2008 *(The Human DNA Regulation Act, 2008),* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa salamu za pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, kwa kuondokewa na mpenzi wao. Aidha, ninatoa pole kwa familia za Wananchi wote wa Kisiwa cha Pemba na Tanga, ambao wapendwa wao walikuwa wakisafiri kwa chombo kilichopata ajali baharini tarehe 14 Aprili, 2009. Yote haya ni mapenzi ya Mungu; Mwenyezi Mungu awape wafiwa wote moyo wa subira na ustahimilivu, pia azilaze roho zao wale wote aliowachukua mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri wa Afya, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Aisha Kigoda (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara, pamoja na timu nzima ya Watendaji, kwa kazi waliyoifanya na kuleta Muswada huu muhimu ili kukabiliana na ubabaishaji wa kukwepa majukumu na kubambikiza watu tuhuma zisizokuwa zao. Matumaini ya Kambi ya Upinzani ni kwamba, Muswada huu unaweza ukawa ni kichocheo muhimu katika kuhakikisha haki na usawa unapatikana katika nyanja zile ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zikilalamikiwa na wananchi wanyonge wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na Muswada. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza marekebisho yafuatayo ili kuongeza tija katika utekelezaji wa sheria:-

Kwanza, kabla ya kupitia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona vinahitaji kufanyiwa kazi, tunamtaka Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi kuhusu sheria ambazo tayari zimekwishaunda mamlaka zinazohusu tafiti. Mamlaka hizo ni *National Institute for Medical Research (NIMR),* ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya. Moja ya kazi zake ni kuangalia tafiti zinazohusiana na DNA ya binadamu. Vilevile kuna Kamati Maalum inayojulikana kama *Medical Research Coordinating Committee (MRCC).* Aidha, kuna *Commission* ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH),* ambayo ndiyo mamlaka inayotoa vibali vya kufanyika kwa tafiti zote za kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoeleweka kuwa *Ribonucleic Acid (RNA), conveys genetic information and catalyzes important biochemical reactions similar, but not identical, to DNA.* Hivyo basi, mtu yeyote anaweza kufanya tafiti ya *RNA*; na kwa kuwa hakuna sheria yoyote inayotoa mwongozo ni nini kinatakiwa kufuatwa na katika mazingira yapi, hivyo basi, mtafiti yeyote anaweza kufanya tafiti hiyo ya *RNA* na akapata matokeo kama yale ambayo yangepatikana wakati akifanya utafiti wa *DNA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inashauri sheria hii vilevile izingatie suala la *RNA* kuwekewa mwongozo kama vile *DNA.* Hivyo basi, tunashauri kiwekwe kifungu kinachosema kuwa, *for the purpose of this Act, RNA is considered equivalent to DNA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu uko kimya kuhusu masuala ya utatanishi wa tafiti za *stem cell* na *genetic engineering* kwa kutumia *DNA* ya binadamu. Kambi ya Upinzani inaona ni bora Muswada huu ukaweka mwongozo kwenye tafiti za aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 2 cha Muswada huu, kinaonyesha kuwa matumizi ya Muswada huu ni upande wa Tanzania Bara tu. Huu ni ukweli uliowazi kuwa, wanufaikaji wakuu wa matumizi ya Muswada huu ni Jeshi la Polisi na Jeshi la Polisi ni chombo cha Muungano. Muswada huu katika matumizi yake ni vyema basi ukafanya kazi pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4(2) kinasema kuwa, Mkemia Mkuu wa Serikali, kwa mujibu wa ofisi yake basi ndiye awe *Regulator*. Kambi ya Upinzani inaona *Regulator* awe ni mtaalam wa *Molecular Biology* au *Biochemistry,* kwa vile kifungu cha 5(e) kinamtaka *Regulator* awe mratibu wa sera, tafiti na mipango yote ya *DNA* ya binadamu Kitaifa na Kimataifa. Hali halisi ni kwamba, Mkemia Mkuu ni mtaalam wa kemia tu na anashughulika na *DNA* ya binadamu katika nyanja za makosa ya jinai *(forensic analysis)* na nasaba ya mzazi na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 11 kinazungumzia uteuzi wa wakaguzi *(inspectors),* kuwa ni maofisa kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Kambi ya Upinzani, inaona si vyema wakaguzi wote wakatoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni vizuri watoke kwenye ofisi au maabara yoyote ya umma inayoshughulikia utafiti wa *DNA* ya binadamu na sifa zao *(qualifications)* zitambulike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 15 kinasema kuwa, kutakuwa na Maabara ya *DNA* ya binadamu katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Muswada huu unaonyesha kuwa, uwezo na madaraka karibu yote amepewa Mkemia Mkuu wa Serikali. Kambi ya Upinzani, inauliza ni nani basi atakuwa na uwezo wa kufanya *check and balance* kwa Maabara hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19 kinasema kuwa, leseni au kibali kitakachotolewa katika Muswada huu kitakuwa cha miezi 12; muda huu ni mfupi. Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa kwa vile tafiti za *DNA* ya binadamu zinaweza kuchukua hata miaka sita; hivyo, kwa vile *regulator* atakuwa anafuatilia kwa karibu tafiti hizo na kwa kuwa kifungu cha 20 kinampa madaraka ya kusimamisha kwa muda au kuzuia kabisa tafiti hizo; muda wa leseni au kibali uongezwe zaidi ya miezi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28(2)(j) kinachosema kuwa *counseling services may be available*; Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Tanzania tumetia saini *Council for International Organization of Medical Sciences (CIOMS)* na *Nuremberg Convention,* ambayo inasema *counseling* iwe ni lazima *(must),* kwa kipimo chochote; hivyo, *genetic test* ni mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 30(3) kinasema kuwa *intimate samples* zichukuliwe na wahusika walio na jinsia sawa na wale wanaochukuliwa sampuli tu. Kambi ya Upinzani inaona sheria haikuzingatia ukweli kuwa madaktari na wauguzi, muda wao wote wawapo kazini wanawahudumia wagonjwa wa jinsia tofauti na wao na kazi inafanyika, kwani watu hao kwa mujibu wa taaluma yao wanakula viapo vya kazi hizo. Hivyo basi, itakuwa ni vyema kama sheria itawaondoa madaktari na wauguzi

katika uchukuaji wa sampuli katika kifungu hicho na badala yake kifungu hicho kiwahusu wale tu ambao hawana taaluma ya udaktari na uuguzi wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 38 kinachohusu *regulator* kutoa kibali *(permit)* cha kufanya utafiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa utaratibu mzima kama Muswada unavyotaka, kifungu hiki kinatakiwa kiangaliwe kwa undani zaidi ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza kwa asasi za *COSTECH, NIMR, TFDA na Regulator* ambaye ni Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unaonyesha kuwa, mtu anayetaka kufanya utafiti anatakiwa kuomba kibali kutoka kwa *regulator,* ambaye ni Mkemia Mkuu wa Serikali. Hivyo basi, kwa mkanganyiko wa asasi hizo zote ambazo zipo kisheria ni bora Mheshimiwa Waziri akaweka bayana ni mamlaka ipi inakuwa juu ya mwenzake linapokuja suala la utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 44(1)(b) kinachosema kuwa *within three months destroy the samples for human DNA collected,* Kambi ya Upinzani inauliza kama taarifa iliyopatika na mtafiti anaitilia shaka na inamlazimu kurudia tena kuchukua takwimu upya. Je, katika mazingira kama hayo ni mpaka atume maombi mapya kwa *regulator?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 59 kinasema kuwa, *Regulator* ndiye atakayeanzisha *data base* ya *DNA* ya binadamu na *data* hizo zitabaki kwake na kutunzwa kwa hali ya usalama na usiri mkubwa. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa hii maana yake ni kuwa itakuwa ni *data base* ya Taifa? Kama ndiyo hivyo, taarifa zote zinazohusiana na kutafuta ufumbuzi wa kihalifu zinakuwa chini ya Jeshi la Polisi, kwani *data base* hiyo ni chombo muhimu sana kwa kutambua watuhumiwa na kurahisisha ukamataji wa wahalifu na hii ni nyenzo muhimu ya kurahisisha upelelezi wa kipolisi. Sasa kama taarifa hizo zote zinabaki kwa *regulator* hii inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dunia ya leo ni ya ushirikiano katika nyanja zote, hivyo sheria tunazozitunga zitilie maanani ushirikiano wa kimataifa. Muswada huu hauzungumzii chochote kuhusu kusafirisha *DNA* ya binadamu nje ya nchi.

Kambi ya Upinzani inaona kwamba, ikilazimu kufanya hivyo, Muswada huu uwe na kifungu kinachotoa mwongozo wa namna usafirishaji huu utakavyofanyika *(Material Transfer Agreement - MTA)* na pia kiwepo kibali cha taasisi itakayopokea *DNA* hiyo nje ya nchi na hivyo, ziwekwe taratibu zitakazodhibiti kadhia hiyo *(Standard Operating Procedures - SOPs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa machache hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuruni Wabunge wote kwa kunisikiliza na ninaomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, kwa kutoa maoni ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasikiliza wasemaji hawa wakuu wawili; yaani Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ninaomba sasa niruhusu mchango wa jumla kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Ninayo orodha ya wachangiaji kadhaa hapa mbele yangu, nitaomba nianze kwa kumwita Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Mheshimiwa Raynald Mrope ajiandae, halafu Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami atafuatia.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu ulioletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Afya. Kwanza, kwa niaba ya Wananchi wa Kongwa, naomba nitoe salamu za rambirambi kwa Wananchi wa Busanda, Wilaya ya Geita, kwa kufiwa na Mbunge wao, ndugu yetu na rafiki yetu Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, tuliyekuwa naye hapa Bungeni. Naomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, nimpongeze Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa Muswada huu wa Vinasaba vya Binadamu wa Mwaka 2009, kwa maandishi ya hapa 2008. Nampongeza Waziri, najua kazi hii hakuifanya peke yake, nawapongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Aisha Kigoda, Katibu Mkuu na Wataalam wote Wizara ya Afya, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya mpaka wakafikia mahali pa kutuletea sheria hii, ambayo inaweka mwongozo kuhusiana na suala zima la matumizi ya teknolojia ya DNA kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii *DNA* kiswahili chake hakijapatikana vizuri, basi tunatumia neno hilo hilo ambalo ameeleza hapa Profesa ni *Deoxyribonucleic Acid ;* ni *genetic material* ambayo ipo kwenye cell ama kwenye *mytocondria,* ambayo inarithiwa nusu kwa nusu kutoka wazazi wote wawili kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kitu hiki kipo kwa binadamu, mimea na wanyama; kwa kifupi viumbe hai. Sheria tuliyoletewa leo ni kuhusiana na mwongozo wa namna ya kushughulika na *DNA* ya Binadamu. Kwa hiyo, wito wangu wa kwanza kwa Serikali ni kwa Idara nyingine katika maeneo yao husika nazo ziangalie matumizi ya *DNA* katika maeneo yao. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo, kuna umuhimu sana wa kuangalia namna *DNA* inavyoweza kutusaidia kuondokana na baa la njaa. Sisi katika Wilaya ya Kongwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla, mwaka huu tuna ukame mkubwa kwa sababu tumepata mvua chache, lakini inawezekana kabisa kwa tafiti hizi kupitia *DNA* za mimea mbalimbali, tukaweza kupata aina za mimea ambazo zinahimili ukame, kwa mvua chache sana tukaweza kuvuna mazao mengi zaidi.

Kwa hiyo, natoa wito kwamba, pamoja na Wizara ya Afya kutuletea hili, lakini sasa na Wizara nyingine ziangalie mchango wa kitu hiki kinachoitwa *DNA* kuendeleza utafiti wake katika maeneo hasa ya hifadhi ya chakula, tuweze kuwa na chakula cha kutosha. Katika dunia ya leo, kutokana na tafiti hizi za *DNA* na nyingine za namna hii za vinasaba, wenzetu wanaweza kukuza nguruwe kwa miezi mitatu toka amezaliwa mpaka akiwa sokoni. Unaweza ukawa na kabichi kwa wiki tatu toka imemea mpaka ikiwa sokoni. Kwa hiyo, teknolojia hii inaweza kutusaidia sana katika kujibu masuala mengi

sana, ambayo yanaweza kutibu suala zima la lishe kwa watu wetu kwa sababu ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili la *DNA* ya Binadamu, kwanza, ningempongeza Profesa kwa kuwa amepanua wigo wa neno binadamu. Lile neno ambalo limetumika kwenye sheria (*Human DNA)*, amepanua wigo; badala ya binadamu huyu tunayemwona kwa macho, lakini yeye amehusisha na ile mijadala ambayo ipo sehemu nyingi duniani kwamba; je, mimba nayo ni binadamu, ambayo wenyewe wanaita *fetus*?

Ukirudi nyuma, amekwenda kwenye *embryo;* ni kitu kuanzia pale mimba inapotungwa mpaka kiumbe kinapotoka kwenye hiyo *embrionic stage* na *stage* ya katikati ambayo ipo humu wanaita *extracorporeal embryo*. Kwa hiyo, wamechukua *stage* zote tatu kabla ya binadamu kuanza kuonekana katika hali yake ya ubinadamu. Kwa hiyo, sheria hii inamkinga mwanadamu kuanzia mimba inapotungwa mpaka anapokuwa binadamu kamili. Hili nalipongeza kwa sababu ya uono huo mpana wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa binadamu, teknolojia hii ina faida kubwa sana; imeelezwa hapa na Mheshimiwa Waziri na Kamati pia imeeleza. Itatusaidia sana katika baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakisumbua. Kwa mfano, masuala ya ubakaji; tukishafika mahali tukawa na *DNA Data Bank* ya nchi nzima, tukawa na watu wetu waliokuwa *mapped* mle na takwimu zao zipo kwenye *computer;* ni rahisi kwa mtu aliyebakwa kuchukua *sample* ile na kuilinganisha na kupata ni nani hasa aliyefanya jambo hilo. *Sample* hiyo ya ubakaji, hata kama ni ya nywele au mate, chochote kile ambacho kitasaidia ku-*link* kuonyesha kwamba ni nani amefanya tendo hili.

Kwa maana hiyo si ubakaji tu, lakini vilevile ujambazi. Matatizo mengine mengi ya jinai yanaweza yakajibiwa kwa teknolojia hii kukaa sawa sawa, tunatambua hilo sana. Vilevile imeelezwa hapa, hata kama watu wamekufa kwa moto hawatambuliki kama *Data Bank* ile ipo ni rahisi kuchukua *sample*, ukalinganisha na ukajua maiti hii ni ya nani. Wenzetu wa Uhamiaji wanatumia sana. Katika nchi za wenzetu, kabla hujahamia kule wanachukua kidogo ili angalau kuweka kumbukumbu vizuri, kuweza kuangalia huyu mtu anayekuja hana magonjwa ya ajabu ajabu ya kurithi, ambayo anayo au mambo mengine ya kiusalama ambayo wanaweza kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumekuwa na matatizo mengi hasa Vijijini na Mijini pia kwamba, mtoto anazaliwa halafu kunatokea ubishi; mababa wawili kila mmoja anasema huyu mtoto ni wa kwangu. Imetokea hata kwenye Biblia, upo mfano ambapo Mfalme Suleiman alipata mtihani mkubwa sana, ambapo akina mama wawili walikuwa wakigombania mtoto, ingelikuwepo teknolojia hii wakati ule jibu lingepatikana haraka sana. Yeye alitatua jambo lile kwa utaratibu ule ambao sote tunaufahamu. Kwa hiyo, kwa akina mama au akina baba ambao watakuwa wanagombea au wanabishania kwamba mtoto huyu wa nani; ni rahisi kupitia teknolojia hii kuweza kujua mtoto huyu ni wa nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti mbalimbali zitakuwa zimepata mahali pa kuweza kupata takwimu zaidi, hasa takwimu za magonjwa ya binadamu hasa ya kurithiwa toka katika kijiji kimoja hadi kizazi kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti nyingine kwa mfano, kuna watu hawapati magonjwa fulani fulani, kuna mtu anakwambia mimi toka nimezaliwa sijawahi kuugua malaria; sasa ni kuangalia hizo *DNA* zao, hivi hawa wenzetu kuna nini; katika kufanya *study* za namna hiyo unaweza ukapata tiba ya malaria ya uhakika. Yupo mtu hapati UKIMWI, huwa haisemwisemwi sana lakini ni kweli kuna watu hawapati; sasa ukitazama *DNA* zao ukajifunza kule unaweza ukagundua kitu fulani ambacho kitasaidia kupata *breakthrough* ya matatizo haya ya maambukizo ya UKIMWI na magonjwa mengine ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna faida nyingi; kuna watoto wanazaliwa wakiwa na jinsia zote mbili na inakuwa haijulikani kwamba huyu mtoto ni wa kike au ni wa kiume; kwa kutumia *DNA* ni rahisi kujua. Mtu anaweza akaona jambo hili kama ni la utani, lakini limetokea Kenya; miezi miwili, mitatu, iliyopita walikuwa na mfungwa ambaye bahati nzuri au mbaya ana jinsia zote mbili. Alipofungwa akapelekwa kwenye gereza la wanaume, akapata matatizo makubwa sana kule, akalalamika sana wakawa wanafikiria kwamba wamhamishie gereza la akina mama, lakini wakawa na wasiwasi anaweza akaleta madhara gani tena kule. Kwa teknolojia hii unaweza ukatambua yule mfungwa ni mwanaume au ni mwanamke na kwa hiyo akapata haki zake za kufungwa upande ule ambao anastahili kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa mifano hii yote kuzungumzia umuhimu wa kitu hiki ambacho Bunge letu leo limeletewa na Mheshimiwa Waziri wa Afya kwamba ni jambo muhimu kabisa katika Jamii yetu na Waheshimiwa Wabunge tulipokee, tuliunge mkono liweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba, ofisi ya *regulator* ianzishwe; natofautiana sana na Msemaji wa Upinzani kwa sababu amepinga isiwe kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Mimi naunga mkono kabisa kwamba, pale ndiyo mahali pake, yeye ndiye *regulator* ataweka Ofisa wake kule ndani, kwa sababu ile ofisi hasa ndiyo itakayokuwa na maabara ambayo tutaitegemea kitaifa kwa ajili ya kumbukumbu hizi muhimu na nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa niseme kwamba, Mkemia Mkuu anapopewa na sheria hii nafasi ya kuruhusu maabara za watu binafsi kufanya kazi katika nchi yetu, hapo napata wasiwasi kidogo, kwa sababu jambo hili tunaloliongelea ni nyeti; kwa nini tusingeenda nalo kwanza miaka minne hadi mitano sisi Serikali halafu baadaye tukiona halina matatizo basi tutafungua wigo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imewekwa *provision* humu kwamba, *regulator* anaweza akatoa kibali hicho. Sasa ushauri nilioutoa hapo mwanzo ni kwamba, *regulator* asitoe kibali kwanza mpaka tutakapojiridhisha, Serikali yenyewe ishughulike na jambo hili, mpaka tutakapojiridhisha kwamba na sekta binafsi nayo inaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Muswada, napongeza sana kwamba, imeanzishwa *Technical Commitee* ambayo imebadilishwa jina kwenye *amendment* imeitwa *DNA Technical Commitee*, ambayo ni nzuri zaidi. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kukubali mawazo ya Kamati na wadau kwa kufanya marekebisho makubwa sana kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *technical commitee* hii wametajwa wawakilishi wa kutoka *Muhimbili University of Health Sciences*, sina tatizo na hilo; swali langu kwa nini iwe Muhimbili peke yake; vyuo ni vingi na vinazidi kujengwa vingine, hivi mwakani tunategemea kupata kitivo kizima cha masuala ya Tiba na Afya kwa ujumla wake katika Chuo Kikuu cha Dodoma; kwa nini katika Sheria tunaandika kabisa kwamba mwakilishi kutoka Muhimbili, *Microbiology Department* Muhimbili; kwa nini usiseme mwakilishi wa masuala ya *microbiology from a relevant university*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wamemchukua *pathologist* wa Muhimbili na vyuo vingine vinazidi kujengwa? Kwa hiyo, katika sheria si vizuri kuandika neno Muhimbili hata kama mtaiteua Muhimbili, lakini ninyi mkaandika kwamba mnahitaji *pathologist* kwa utaratibu huo, mnahitaji mtu wa *biotechnology*. Mmesema mnayehitaji itabidi atoke *SUA;* kwa nini *SUA* hata *University of Dar es Salaam* pale ipo *department* nzima ya *biotechnology* na vyuo vingine vinaanzishwa kama tulivyosema? Ukiweka katika sheria sasa itakuwa ni lazima atoke *SUA*, kesho na keshokutwa tutaulizwa kwa nini *SUA* tutajibu nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile hapa imewekwa *representative from a privately owned designated laboratory*; ndiyo hizo *laboratory* ambazo mimi siziungi mkono hata kidogo. Kwa nini sasa huyu *representative* awe *private,* afadhali kama wana *organisation* yao sawa, lakini huyo *private* utampataje? Ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake walitazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika sheria hii *sampling officers* kwa sehemu kubwa nimeona ni wale tu wa Mkemia Mkuu; swali langu ni kwamba, hata kwenye *collection*, kwenye *analysis* sawa wana-*analyse* Mkemia Mkuu na *laboratory* zake, lakini kwenye *collection* tuki-*limit* hivyo itatuletea matatizo. Nchi hii ni kubwa na wataalamu hawa wa Mkemia Mkuu hawako kila mahali katika nchi yetu, kwa hiyo, itazamwe wapo wataalamu wengi tu ambao wanaweza kufanya kazi hiyo. Naomba Waziri atakapofafanua asisahau suala la *RNA*, je, nayo itaendana na *DNA* au yenyewe itabaki vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo Muswada uliopo mbele yetu. Kabla hatujafanya hivyo, naomba nami pia niungane na Wananchi wa Masasi katika kutoa pole sana kwa wenzetu wa Busanda, ambao wameondokewa na Mbunge wao, Marehemu Rwilomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa bahati nilionana naye siku moja kabla ya umauti wake kule India, kwa kweli nilipata bahati hiyo ya kumuaga asubuhi yake ndiyo nikaondoka kurudi nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nilikuwa India kwa matibabu. Nataka kuwaeleza ndugu zangu wa Masasi kwamba, nimepata matibabu safi kabisa. Nilikuwa na matatizo kwenye pua kulikuwa na uvimbe lakini umeondolewa vizuri kiasi kwamba hata ukiniangalia hakuna hata alama unayoweza kuiona puani kwangu kama nimefanyiwa *operation*. Teknolojia waliyoitumia ni ya kisasa na ninawashukuru sana Serikali hasa Wizara hizi mbili za Afya pamoja na Bunge, kwa kuniwezesha kuwepo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani zangu hizi, naomba sasa nimpe pongezi Waziri wa Afya, pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watumishi wa Wizara hii, kwa kuuleta Muswada huu mbele yetu. Muswada ni safi sana, nami katika kuchangia nataka kusema kwamba si rahisi sana kwa watu au wananchi wa kawaida kuuelewa, kwa sababu huingilia sana kwenye mambo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niuelezee kwa lugha ambayo wananchi wangu wa kawaida wanaweza wakaelewa. Niseme kwamba, hasa kwa kule kwetu Kusini kwa makabila ya Wamakua, Wayao, Wamwera na Wamakonde, hawa walikuwa na dhana toka awali ya kimila kwamba, mtoto yeyote anayezaliwa ni mali ya mama. Dhana hii inatokana na imani ya Wamakua na Wayao kwamba, mama ndiye mwenye uhakika wa uzazi wa mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama ndiye anayezaa na kunyonyesha, kwa hiyo, ana uhakika na ukoo huo lakini kwa upande wa baba kuna maswali mengi; wakati mwingine unaweza kukuta baba amepachikiwa tu mtoto si wake, lakini basi anakubali tu kwa ile dhana ya kusema kwamba kitanda hakizai haramu. Kitanda hakizai haramu, shauri yenu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili waliliona toka mwanzo wakaamua ukoo unatokana na huyu mama na baadaye makabila makubwa duniani kama Waisrael, Wafilipino, Wanaijeria nao wakaikubali dhana hii.

Nataka kuielezea hii ili niweze kuunganisha kwa upande huu wa *DNA,* suala hili limekuja baadaye kwenye miaka ya sitini na liligunduliwa na wataalamu wa Kimarekani wanaoitwa *Watson* na *Crick;* hao ndiyo wagunduzi wa *DNA*. Wagunduzi hawa ndiyo waliokuja kuwakomboa wanaume, kwa sababu kwa mara ya kwanza ilieleweka kwamba kuna chembechembe zinazotoka kwa baba na kwa mama, hizo peke yake ndiyo zenye uhakika katika uzazi wa mtoto. Kwa hiyo, kuanzia ile miaka ya sitini wanaume wakajidai kweli kweli kiasi kwamba, hata mila zetu sisi, kwamba mtoto ni mali ya mama zikaanza kufifia na siku za karibuni zimekufa, tumebaki sisi na majina yetu tu. Mimi naitwa Mrope, huu ni ukoo wa mama yangu; kama ingekuwa nifuate mambo ya siku hizi ningekuwa naitwa Mmole. Vilevile Mheshimiwa Rais Mstaafu anaitwa Mkapa kutokana na kuzaliwa na mama, lakini kama ingekuwa leo hii tufuate haya yaliyoletwa na akina *Watson* na *Crick,* basi naye angekuwa anaitwa Matwani. *(Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona hili niwaeleze wenzangu na hasa wa kule kusini kwamba, kumbe na sisi dhana hii tulikuwa tumejifunza zamani na tukaanza kuizoea katika mila zetu, hivi leo tusizoee sana juu ya hii *DNA* iliyokuja sasa; *DNA* kama tunavyoifahamu, kweli ni dhana nzuri lakini hebu tuangalie ni jinsi gani matumizi yake yanavyoweza kuboreka, kwa sababu hatari ya *DNA* ni kwamba, kama ikikutana na watu ambao wana nia mbaya na si waaminifu, haya mengi yaliyotajwa katika Muswaada huu yanaweza yakavurugika kabisa. Tukiwa na watu waaminifu, wanaoelewa sawasawa, *DNA* ni dhana mojawapo ambayo ni nzuri sana na itatuondolea matatizo mengi na hasa eneo la uhalifu nalo linaweza likadhibitiwa kutokana na hii teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa watu wengi hasa katika nchi za Afrika wanaitumia *DNA;* mimi naweza kusema kwamba wanaitumia vibaya, wanaifananisha zaidi na masuala ya uzazi ambao si halali. Kila mtu anafikiria kwamba, labda nimesingiziwa kuzaa na binti fulani na wanaume wanataka wahakikishiwe kama yule mtoto kweli ni wake na kadhalika. Mimi nasema kwamba, hapa tunaweza kutumia teknolojia hii tukawabana sawasawa wale mababa wanaowapa mimba watoto wetu wa mashuleni; kwa sababu mara nyingi wakibanwa huwa wanakataa, sasa tumekuja mahali ambapo tunaweza kuwapeleka katika maabara hizi za *DNA;* tukithibitisha kwamba yule mtoto ni wake kutokana na *DNA*, basi huyu baba anastahili kufungwa maisha au miaka 30, kwa sababu ya kumwingilia mtoto ambaye alikuwa bado hajawa na umri ule wa kuweza kuzaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni mojawapo ambalo linaweza likatumika vizuri tu. Papo hapo ninaomba sana Wizara hii ya Afya, iangalie uwezekano wa jinsi ya kuwa na maabara za *DNA* katika Kanda ili kesi zinazotokea katika mikoa hiyo zichunguzwe huko huko badala ya kuzipeleka zote Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yangu kubwa ilikuwa kuunga mkono hoja hii na kusema kwamba, ikitumiwa vizuri itasaidia. Naamini Muswada huu tutaupitisha ili tuweze kukamilisha mambo mbalimbali, ambayo yamo katika Muswada na ambayo nchi yetu inaweza ikafaidika moja kwa moja kutokana na kutumia hii teknolojia ya *DNA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mrope kwa mfano wako, ingawa hujajitolea mfano na wewe ungeitwa nani kama ungefuatwa utaratibu huo.

**MBUNGE FULANI:** Amesema.

**MWENYEKITI**: Amesema eeh! Basi tunakushukuru sana.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, nami nitoe mchango kidogo kuhusiana na Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu, kutoa rambirambi zangu kwa Wanajimbo la Busanda, kwa kuondokewa na Mbunge wao, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba; Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri na wenzake wote, walioshirikiana kwa pamoja katika kuandaa Muswada huu ili iwe sheria inayohusiana na masuala ya *DNA*. Muswada umeandaliwa vizuri na kwa ujumla wake kwa kweli umechelewa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ingekuwa imekwisha kutungwa tangu zamani, lakini pamoja na hilo daima kwa nchi yetu huwa nasikitika kitu kimoja, kuna sheria nyingi nzuri lakini utekelezaji wake ni kama haupo. Sheria tunaiweka, tunaitunga inakuwa na misingi mizuri, tunaweka hata *regulations* zake; nenda kwenye utekelezaji wake, pengine hata asilimia ishirini ya sheria yenyewe inayohusika haifiki, ndiyo tatizo tulilonalo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingi kama ambavyo nafikiria hata sheria hii pengine inaweza ikakumbana nayo ni suala zima la uaminifu; rushwa bado inaweza ikatumika katika kukomoana; hatujadhibiti vizuri suala la rushwa katika maeneo mengi yanayohusiana na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ni nzuri sana, inatoa haki kwa yule anayeonewa na kunyanyaswa. Vilevile vyombo vinavyotoa haki hiyo, mara nyingi ndiyo vimekuwa vikiongoza kuikandamiza haki kwa rushwa; iwe Mahakama au iwe Polisi. Hata tutakapokwenda hospitali kupima, bado ukandamizaji huo unaweza ukawepo; maana yake tunaanza kutazama ni nani anayepeleka *sample* hiyo na uaminifu alionao, kwani yule anayepima anaweza akageuza matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko zinakopelekwa badala ya kupeleka damu ya Ponsiano Nyami, samahani nitamtaja jirani yangu, ikapelekwa damu ya Mheshimiwa Mwananzila; majibu yatakayokuja ni ya Mwananzila lakini tunayasadiki kwamba ni ya Ponsiano Nyami. Rushwa inaweza ikatumika pia na watakaoumia zaidi bado ni wale ambao hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona leo hii hata baadhi ya *advocates* unamlipa akutetee kwenye kesi yako, lakini huyo huyo anageuka kukunyanyasa na kukuhujumu kupata haki yako; hahudhurii mahakamani. Vyombo vinavyohusika vinapokuja kumfutia yale mamlaka ya kuendesha kesi, baadaye anazunguka anahonga wanamrudishia haki hiyo na anaendelea kunyanyasa wateja wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukasema asilimia tisini hata mia moja kama tunashuhudia mtoto ni wa mama kabla hatujathibithisha asilimia mia moja nyingine kwamba, huyu mtoto kazaliwa na baba huyu. Kwa hiyo, ndiyo maana sina hakika, lakini nadhani ndiyo ikaja pengine hata ile dhana ya kusema kitanda hakizai haramu. Mama ana uhakika kwamba ni mtoto wake kwa sababu kitanda hakizai haramu.

Vilevile kuna sheria za baadhi ya dini, ambazo kama nimeoa pengine nimekwenda kusoma mtoto amezaliwa ndani ya ndoa; mtoto yule ni halali, huwezi ukamwita nje ya ndoa wakati amezaliwa ndani ya ndoa.

Sheria yangu inakubali na kwa hiyo nikiamua kukataa kwamba huyu si mtoto wangu lakini pengine sheria ya dini yangu inanibana kwamba huyo ni mtoto wangu, ni kosa mimi kwenda kulalamika kwamba si mtoto wangu tukapime *DNA*, maana hata nikifa mtoto yule ataruhusiwa kunirithi. Kwa hiyo, sheria zetu pia zinapokwenda hivyo, zijaribu kutazama haki na sheria mbalimbali za jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema Mkemia Mkuu wa Serikali ndiye atakayepewa mamlaka makubwa ya upimaji huo; hilo sipingani nalo, lakini nilikuwa nashauri kwamba, tunazo hospitali za rufaa hasa zile kubwa kama Bugando - Mwanza, KCMC - Moshi, tunayo Hospitali ya Mbeya na hata ya Jeshi Lugalo, nazo hizi zingeruhusiwa kupelekewa wataalamu hao na huko pia upimaji ufanyike, maana utaalamu ni ule ule na viapo vyao vitakuwa ni vile vile. Kwa hiyo, itarahisisha kutokuwa na msongamano wa upimaji wa *DNA* katika eneo moja, maana nchi yetu sasa ina watu zaidi ya milioni thelathini na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofikiria kupeleka eneo moja tu; sisi ni watu wa namna gani, maana yake ni kwamba hatutambui na wala hatuthamini uwezo tulionao na wala hatutaki kupanua wigo; tunataka mtu mmoja tu, matokeo yake tutajenga mazingira ya rushwa kuendelea. Huu ni ukiritimba ambao hauna sababu, tutazame kuhusu sheria ya makosa yenyewe.

Endapo mimi nilikuwa ninabisha kuwa huyu si mtoto wangu, lakini vipimo vimeonyesha kwamba huyo hakika ni mtoto wangu: Je, kuna sheria ipi ambayo itanilazimisha sasa kutekeleza lile ambalo limekusudiwa lifanyike kama ni fidia kubwa, kama ni matunzo kuwa makubwa au vyovyote itakavyokuwa, ni sheria gani ambayo imewekwa kumbana mhusika aweze kuwajibika kikamilifu?

Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kasema sheria mbalimbali za idara mbalimbali zitarekebishwa baada ya sheria hii kupita; ametaja uhamiaji, ametaja polisi, ametaja na maeneo mengine, kwa muda gani?

Namshukuru mchangiaji aliyepita - Mheshimiwa Mrope, ametaja suala la wanafunzi wanaopewa mimba. Wengi wanapewa mimba na ni tatizo la Taifa letu. Lakini walio wengi wanagoma. Wote wanagoma! Kuna kipengele gani kinacholazimisha kwamba kwa wanafunzi wote watakaokuwa wamepata mimba na wakamtaja mtu, mtu huyo akakataa kwamba sasa ni lazima damu yao ipimwe? Kipengele gani kitakuwa kimetaja hapo kumbana?

Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, kipengele hicho mkiweke kukitilia maanani tatizo tulilonalo leo hii. Lazima wawepo watu fulani ambao watalazimishwa kupima *DNA*, ninaamini kwamba ndoa nyingi zitaimarika kwa sababu kutakuwa na uaminifu kwa pande zote mbili. Kwa mwanaume na hasa kwa wanawake.

Ninaamini pia kwamba hata uholela wa watoto wa Mitaani utapungua kwa sababu watu wataogopa kwamba nikimpa mwanamke mimba na nikakataa yule mtoto damu yetu itakwenda kupimwa. Lakini pia itaweka uaminifu kwa wanawake ambao leo yuko hapa, kesho yuko pale, keshokutwa yuko pale na hajui nani kampatia mimba. Kwa hiyo, nayo hiyo itaweka nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Menyekiti, naamini uaminifu utatawala sheria hii nzuri, lakini isiwe ni sheria ya kuweka kapuni kama tunavyofanya katika sheria nyingi. Nani anayejali sheria Tanzania? Naunga mkono sheria hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Lakini kwa kweli sheria hii itatoa usawa kwa pande zote mbili kwa wanaume na wanawake ili kuwa na mwelekeo sahihi wa watoto ni wa nani si itawadhibiti wanawake peke yao hata wanaume pia. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Naimi kadhalika kwa niaba ya wananchi wa Ludewa natoa rambirambi kwa wenzetu wa Busanda kwa kupotelewa na Mbunge wao. Lakini vile vile kuna ndugu zetu walipoteza maisha katika Bahari ya Hindi, wakati boti likitoka Tanga kwenda Pemba lilipoungua na kuzama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa nguvu zote. Naunga mkono kwa sababu natambua umuhimu wa Muswada huu. Bila kutoa maelezo marefu nadhani wenzangu wamechangia vizuri tu. Lakini yatosha kusema ni Muswada muhimu, ni Muswada wa kisasa tunakwenda na wakati katika karne ya 21 ya sayansi na teknolojia. Nchi nyingine walianza siku nyingi sana kuwa na sheria hizi na sisi leo tunaingia katika mkumbo huo. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watalaam wote walioleta Muswada huu mzuri uliokuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ila nilitaka maelezo kutoka kwa Waziri atakapokuwa anajumuisha katika mambo machache.  Nina mambo manne.

La kwanza, katika Muswada huu ukurasa wa 19 kifungu cha 30(3) ambapo tunazungumzia ukusanyaji wa kinachoitwa katika kimombo *intimate sample, particularly* anapokuwa ni mtu mwenye jinsia ya kike, yawezekana sikuelewa, lakini kama nimeelewa, nadhani kifungu hiki kinataka *collector* anayekusanya *samples* hizo awe ni wa jinsia hiyo. Hapa kinazingatia, jinsia ya kike kwamba kuwe na *collector* ambaye ni wa jinsia hiyo. Nikadhani ni kifungu cha ubaguzi sana hiki, kwa sababu kama ni suala la *intimacy,* basi iko  hata wanaume wanapochukuliwa *intimate samples* wachukuliwe na wenzao wa jinsia hiyo na sioni iwe ni kwa wanawake tu kwa sababu *intimate* iko *on both sides*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua imerekebishwa kidogo kwenye marekebisho yaliyotolewa, lakini bado naona hoja iko pale pale, inazungumzia kwamba mwanamke ndiyo ashughulike kuchukua *intimate sample* kutoka kwa mtu wa jinsia hiyo. Nilidhani

*after all* tumeambiwa watalaam hawa wanaochukua *samples* wamesomea mambo haya, wameapa, kwa hiyo, hakuna sababu ya kuwa na matatizo na kusema lazima awe mtu wa jinsia fulani. Lakini kama ni lazima, basi tuwe *fair* kwa pande zote mbili na wanaume vile vile wachukuliwe *samples* na wanaume wenzao kama itakavyokuwa kwa akina mama.

Kwenye ukurasa huo huo wa 19 kifungu cha 33 kinazungumza kuhusu usafirishaji wa *samples* na kwamba namna itakavyosafirishwa ile *mode of transportation* iwe ni maamuzi ya *collector* kwa kuzingatia; najua kifungu kinachofuata 33 (2) kinatoa maelekezo zaidi, lakini bado naona kungetolewa maelezo katika asiachiwe mtu mmoja kujiamulia atasafirisha vipi kwa sababu ni *sample* za muhimu sana *(very sensitive samples).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mtu ajiamulie yeye kwamba nitasafirisha kwa punda, kwa pikipiki eti kwa kuzingatia mazingira anayoyaona yeye *no, no! I think* isemwe wazi kwamba mazingira mazuri, *experience* hata kutoka kwenye nchi nyingine wanafanyaje? *DNA sample* inabebwa hivi hivi kienyeji na mtu mmoja anajiamulia au kuna taratibu zake? Ndiyo nilitaka nipate ufafanuzi mzuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwenye hilo. Hofu yangu ni kwamba asije mtu akaamua kubeba tu kwa njia ya punda halafu akaviziwa njiani akanyang'anywa akasema zimepotea kumbe amezipoteza. Siyo kwamba zimepotea, bali amepoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu nilitaka kuzungumzia kwenye ukurasa wa 33 kile kifungu cha 71 (2) hapa suala ambalo naambiwa *without prejudice* Waziri atatakiwa kufanya. Kuna vitu mbalimbali pale, anapewa majukumu Waziri kuyatekeleza. Sasa niko kwenye kifungu kidogo zaidi cha (e) kuhusu *disposal* ya *human wastes* baada ya kufanya *laboratory test*, takataka zile zilizotumika zinakuwa *disposed* vipi. Muswada huu unapendekeza kwamba Waziri apewe majukumu ya kuamua nadhani. *In particular and without prejudice to the generality of sub section (1) the Minister shall make regulations.*

Lakini nilitaka kusema kwenye hili la *disposal*, kuna sheria mama ya mazingira ambayo inazungumzia namna yaku-*dispose wastes* za aina mbalimbali *including medical wastes* pamoja na waste za binadamu au wanyama hizo taratibu zipo kwenye sheria hizo nyingine. Nilitaka kujua kwa nini Waziri hafanyi *reference* kwenye sheria hiyo ili kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na sheria nyingine ambazo tumeziweka sisi wenyewe.

Lakini vile vile ya mwisho, samahani nitarudi nyuma kwenye ukurasa wa 24 kifungu cha 48(2) kwenye suala la *incompetent persons*, yaani namna ya kuchukua samples kwa *incompetent persons.* Wawepo watu ambapo ni *parents, gudians, representatives* lakini wame-*add* hapa *social welfare officers, or a community development officer*. Lakini katika Muswada mzima pale ambapo inahusu *incompetent persons* wanaotajwa ni makundi matatu tu, yaani *parents, guidance* na *representatives*. Lakini hapa kuna *social welfare officers or community development officer*.

Nilitaka kujua, nifafanuliwe, kwa nini hapa wameingizwa hawa watu watatu kama wanaweza kumsaidia *incompetent person* katika kuchukua *samples* au kupata *information* inayotokana na *test* hizo? Nilitaka kujua hawa wameingiaje hapa kwa nini hawakuwa wanatajwa *throughout* katika Muswada mzima na kwa nini kwenye kifungu hiki tu hawa watatu wamechomekwa hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa ni wa kutaka ufafanuzi katika hayo, lakini nirudie kusema kwamba Muswada huu ni mzuri, umekuja kwa wakati na mimi naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, Profesa Raphael Mwalyosi alikuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho na kwa mujibu wa taarifa niliyoipata kwa Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, hoja haitachangiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, atachangia Waziri mwenyewe.

Sasa baada ya kuwasikiliza wachangiaji wote nitamwita Mheshimiwa Waziri, aje atoe ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na baadaye tutaingia kwenye hatua nyingine kama muda wetu utakuwa unaturuhusu.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa mara pili jioni hii ili niweze kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo wenzangu wamechangia kwa nia ya kuboresha Muswada huu hasa kwa upande wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuhitimisha hoja yangu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi wote nawashukuru sana kwa michango yao ambao nina imani kubwa itatusaidia wakati wa kutekeleza Sheria hii baada ya kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida naomba niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Omar Shabani Kwaang'w, Mwenyekiti wa Kamati wa Huduma za Jamii, Mheshimiwa Ali Tarab Ali - Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi. Naomba niwashukuru sana kwa michango yao. Vilevile nina Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi, naomba niwatambue. Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Mercy Emmanuel na Mheshimiwa Charles Mwera. Wote nawashukuru kwa jinsi mlivyoisaidia Wizara katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Kwaangw' kwa kukukubaliana na yale maudhui ambayo tumetoa katika mapendekezo yetu ya sheria na ametoa ushauri katika maeneo mbalimbali.

Napenda kusema kwamba yote aliyoyasema yapo katika jedwali la marekebisho. Vilevile alitoa suala la *DNA* na *RNA* ambalo limejirudia na hilo pia lipo katika jedwali letu la marekebisho. Hili pia lilizungumzwa na Mheshimiwa Dr. Tarab Ali Tarab Ali akiangalia kwenye jedwali letu la marekebisho tunapozungumzia *by genetic material* ambapo kwenye ufafanuzi halikuwepo pale awali. Sasa hivi tunasema *genetic material includes human DNA* na *RNA*. Katika vikao vyetu pamoja na Kamati tukubaliana kwamba hiyo inatambua umuhimu wa *RNA* na kwamba ni vizuri ikatamkwa pia katika sheria na imetamkwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Omar Kwaangw' vilevile amezungumzia habari za maeneo mengine ya uchapishaji na hayo tuliyaona hata kwenye Kamati na tunaahidi kwamba sehemu zote hizo kabla Muswada haujafikia hatua ya kupeleka mbele yote yatatazamwa na kurekebishwa maeneo yote ambayo ni ya uchapishaji, ya sarufi na maeneo mengine. Y ote hayo tuliyaona kwenye Kamati na sisi tupo tayari tutayarekebisha kwa jinsi itakavyostahili.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali ambaye ni Mjumbe wa Kamati hii, vile vile niliwahi kumshauri kwamba mengi anayokuja kuyasema hapa ayalete kwenye Kamati ili tuyaweke kwenye majedwali, lakini bado ule ugonjwa unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali alitukumbusha kwamba kuna vyombo kama *National Institute Medical Research* na *COSTEC* ambazo zinafanya utafiti na kwa uelewa wake ni kwamba sheria hii inakuwa kama ina *over shadow*. Sisi tunasema hapana! Ni kwamba hivi vipimo vya *DNA* vya binadamu sasa hivi vinafanywa katika eneo moja kwa upande wa Serikali.

Lakini kuna maeneo mengi sana pia yanafanya *DNA* na hii katika hoja nyingine ambazo Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba tupate uzoefu kwanza kabla hatujatoa vibali kwa watu wengine, ninachosema ni kwamba moja ya chimbuko la kuleta Muswada hapa Bungeni ni kwamba hizi shughuli za tafiti na za kutumia *DNA* zinafanyika katika sehemu nyingi. Muhimbili tayari wanafanya, *University of Dar es Salaam* na Chuo Kikuu cha Sokoine.

Kwa hiyo, tunachotaka ni chombo ambacho kitaratibu na tuweze kuwa na mfumo, siyo kila mmoja anajichukulia. Sasa ndiyo ikaonekana kwamba endapo kutakuwa na watu watataka wawe na *private laboratory,* ndiyo hiki chombo ambacho kitaweza kikawadhibiti, tuwe na *centralize* sehemu ambayo wanaweza wakaja wakaomba ruksa. Tutazame maabara zenyewe ziwe zinakidhi na wataalam ndio hasa ilikuwa nia. Vinginevyo tutaacha itakuwa holela na tunaweza tukajiletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali mimi najua ni Mkemia, amesema Muswada upo kimya kuhusu *stem cell genetic engineering*, lakini hapo hapo anaendelea kusema kutumia *DNA* ya binadamu. Maadam wanatumia *DNA* ya binadamu hatuwezi tukaji-*limit* kwenye *stem cell and genetic engineering* pekee kutakuwa na maeneo mengi ambayo *DNA* ya binadamu itatumika. Kwa hiyo, katika

Muswada si lazima kutaja kipengele kimoja kimoja. Maadam huo utafiti au teknolojia inayotumika, hiyo ya *DNA* ya binadamu ina maana kwamba wapo *bounded* na sheria hii.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali alipendekeza vilevile kwamba huu Muswada kwa sababu Jeshi la Polisi ni wadau wakubwa, basi uwe pande zote za Muungano. Kwa utaratibu Bunge hili likitunga sheria, *application* yake inakuwa huku Bara, lakini Baraza la Wawakilishi likiona ni vyema pia iende upande ule, wanaweza wakachukua maudhui au wakatunga sheria yao. Lakini sheria tunazotunga hapa labda ziwe za Kimuungano ndiyo zinaweza zikaenda pande zote mbili, lakini Baraza la Wawakilishi lina mamlaka kamili ya kutunga sheria zake.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali alisema vilevile kwamba kifungu 42, kinasema Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa ofisi yake ndiye *regulator*. Kambi ya Upinzani inaona kwamba *regulator* awe ni mtaalam wa *molecular biology* au *biochemistry*. Sasa hivi huyu anakuwa *proposed* kuwa *regulator*, ni Mkemia Mkuu ambaye ni Mkemia. Lakini hapa nadhani tusiangalie sura kwa sababu hayupo pale maisha yote, atakayechaguliwa ni mtu yule ambaye tunaona anaweza akafanya kazi nzuri ya *regulator* siyo kuangalia sasa hivi ni Mkemia, lakini baadaye anaweza akawa mtu mwingine kufuatana na jinsi tutakavyowapata watu.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali alisema vilevile kwamba kifungu cha 15 hakionyeshi kama kutakuwa na *check and balances* kwa sababu madaraka yote amepewa Mkemia Mkuu wa Serikali na watu pia katika Kamati yake pia wanatoka huko. Naomba akubaliane na mimi kwamba hili ni suala la kisayansi. Kwa hiyo, *check and balances* zaidi iwe kwenye *quality control* na *quality assurance* na hii naomba nimhakikishie kwamba kwa kutazama jinsi kazi itakavyofanywa na mashine zitakuwaje haya ni masuala ambayo ni muhimu zaidi kuliko kwamba tuwe na mtu mwingine wa kuja kucheki kazi inayofanyika.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali amesema pia kifungu Na.19 kinasema kwamba: “Leseni zitolewe kwa muda wa miezi kumi na mbili” Huu ni muda mfupi. Lakini sentensi yake ya mwisho anapendekeza kwamba muda wa leseni uwe zaidi ya miezi kumi mbili. Mimi ninafikiri kwa kuanzia, kwa sababu hizi teknolojia zipo nchini, hatujui wanafanya kazi kwa ufanisi kiasi gani? Nadhani tungeweka muda mfupi ili mtu anayekuja kuomba leseni upya atuhakikishie kwamba kazi wanayofanya ni nzuri. Nadhani huko mbele ya safari tutaangalia kama tutaanza kuaminiana. Lakini kwa mwanzo kama hivi sasa, nadhani muda wa mwaka mmoja utatosha tupate ripoti kafanya nini na kwamba tumwamini vipi ili kuongezea muda.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali suala lingine alizungumzia habari za *cancelling service may be available.* Ukiangalia kwenye jedwali ni kwamba, hili limekuwa *taken care of* haya katika Muswada, yameelezwa kwamba ni mambo ambayo lazima yawepo na katika jedwali inasema: *Genetic cancelling Services,* haisemi *may be available,* yaani ni mambo ambayo lazima yawepo.

Kifungu cha 30 kinachozungumzia habari za *intimate samples,* hili limezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali pamoja na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi na hii ipo kwenye jedwali ambalo pia Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi amesema limerudia kosa lile lile la kuwabagua wanaume kama nimemuelewa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye jedwali la marekebisho kama utaniruhusu nisome kinasema: "*where intimate sample for human DNA is to be taken from a female personal, a female sampling officer or in her absence any sampling officer who is available shall take the sample for human DNA from that person*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli hapa tumeangalia utalaam zaidi kuliko jinsia. Lakini katika mazingira yenyewe tunaposema *intimate sample* kwa mwanamke ni *real intimate* na tunasema endapo kuna mwanamke ambaye ana uwezo wa kufanya hivyo, basi afanye hiyo kazi. *The only times* ambazo tunaweza tukahitaji *an intimate sample* ni katika kesi za *rape* ambapo unataka kupata *semen* kutoka kwenye maeneo ambayo ni nyeti. Lakini nakubaliana Wabunge wenzangu kwamba hapa tuangalie utalaam zaidi. Lakini hapa tunasema endapo kuna mtalaam ambaye ni mwanamke ngoja tumtumie huyo, lakini ikishindikana, basi tutatumia mtalaam yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Taarab amezungumzia pia kuhusu *database* ambayo katika Muswada tumesema itatunzwa katika maabara ya Mkemia Mkuu. Wazo lake ni kwamba *database* hii watumiaji ni pamoja na mambo ya hali ya usalama na usiri mkubwa na kwamba kwa nini isiwe chini ya Jeshi la Polisi kwa sababu wao ndio wanawatafuta wahalifu? Mimi nadhani kinachohitajika hapa ni kwamba pawe mahali ambapo pana usiri mkubwa na pia pawe *(safe)* pawe pa usalama, halafu kuwe na uwezo wa kupata *information* unapohitaji. Sidhani kama kutakuwa na matatizo ikienda polisi au ikienda mahali pengine. Polisi siyo watumiaji peke yao wa huduma hii. Kwa hiyo, nadhani hilo lisilete mjadala kwamba iko wapi. Ikiwa tutaona kwamba siri zinavuja au hakuna usalama, basi nadhani tuko tayari kuihamishia mahali pengine. Lakini kwa sasa hivi hatuoni umuhimu wa kwamba tupeleke polisi kwa sababu siyo wadau peke yao.

Halafu Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani alizungumzia kwamba hii *DNA* ya binadamu imesambaa kila mahali duniani na kuwe na kipengele cha kutuwezesha kuwe na *materials transfer agreement* tuweze kuwa na mahusiano na maabara nyingine. Sijaona sheria ya namna hii, lakini kwa sababu kuna maeneo mengi ambayo Waziri mwenye dhamana amepewa majukumu itakapobidi nadhani tutaiweka hiyo kwenye *regulation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani ulinistukiza kidogo nilidhani nitamalizia kesho. Mheshimiwa Ndugai ametushauri kama Serikali katika idara nyingine ziangalie uwezekano wa kutumia teknolojia hii katika maeneo mbalimbali akazungumzia habari za kilimo. Nilidhani atataja na minazi ambayo tumezungumzia leo asubuhi nakubaliana naye. Ndiye aliyesema kwamba huyu *regulator* asianze kutoa vibali kwa watu binafsi mpaka tupate uzoefu. Lakini nilitoa hili kwamba tayari kuna maabara binafsi zinatumia kwa hiyo, nadhani wakati muafaka na nikubaliane na Mheshimiwa Ponsiano Nyami aliyesema kwamba tumechelewa. Lakini *better late than never*.

Hili suala la wawakilishi katika Kamati sijui kama amepata nafasi ya kusoma kwenye jedwali letu ukurasa wa tatu, *clause* ya tisa ambayo tumezungumzia *by Representatives from Biochemitry Department of any recognized University in the country, a Representative from the Department of Forensic Pathology,* hii tulizungumzia *National Hospital.* Lakini *Representatives of Biotechnology Department from recognized University, Representatives from the molecular biology and Biotechnology Department of any recognized University in the country.* Kwa hiyo, hili tuliliona na tulisema tusiji-*limit* kwa vyuo fulani ila tuweze kuangalia kwa upana ili tuweze kuwapata watu ambao tunafikiri wanaweza wakatenda kazi nzuri popote walipo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mrope, amezungumzia kwamba *motto* ni "wamama" na hii imeungwa mkono na watu wengi, yeye ndio anajua. Akaleta hoja ya kwamba wanafunzi ambao ni matatizo makubwa katika suala la mimba sasa hivi tunaelekea ukikongi kwa kuwanasa na ninashukuru kwa yeye kuliona hilo kwa sababu maeneo ya Mtwara na Tunduru na kule kwa Mheshimiwa Kawawa, ni maeneo ambayo kuna *drop out* nyingi sana za watoto hasa wa *primary* kwa sababu ya mimba. Tunakubaliana kuwa na kipimo cha namna hii kitatusaidia kuwanasa wale wajanja waliokuwa wanakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, amependekeza kuwa maabara isiwe Dar-es-Salaam tu. Hili suala limezungumzwa pia na Mheshimiwa Nyangoro, kwamba tujaribu kuipeleka hii huduma karibu zaidi na wananchi. Hii ndio sera ya Serikali na ndio sera ya Wizara, jinsi tunavyopata uwezo wa kifedha na wataalamu hatutasita kufanya hivyo. Tumetaja kwa kuanzia, inaweza ikawa kikanda kama vile tulivyo na hospitali za kikanda, halafu baadaye tutakwenda polepole karibu zaidi na wananchi kwasababu ni huduma ambayo wengi wataihitaji, kwa hiyo, ipo haja ya kuwasogezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nyami, alisifu kwamba huu ni Muswada mzuri, lakini wasiwasi wake ni utekelezaji. Lakini wasiwasi wake haukuishia kwenye Muswada huo, anasema sheria nyingi tunazotunga hapa lakini hakusema kwamba tuache kutunga sheria. Lakini nashukuru kwamba aliusifu huu Muswada kwamba umekuja kwa wakati muafaka na umechelewa na kwamba unahitajika. Ameongea kwa kirefu kuhusu rushwa na kwamba watu wanaweza wasiwe waaminifu wakabadilisha vipimo vya huyu vikaenda kwa mtu mwingine na vya kwake vikaenda kwa Mheshimiwa Mwananzila. Niseme tu kwamba suala la rushwa ni pana na tuna vyombo na wote hapa tuko katika mapambano ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hatuwezi kuacha kutunga sheria kwa kuogopa rushwa. Rushwa ipo katika maeneo mengi, ipo katika hospitali, lakini nimhakikishie kwamba watu wanaokula rushwa ni *small percentage,* watu wengi ni waaminifu. Lakini unapokuwa na mla rushwa basi hao ndio wanachafua *institution* nzima.

Kwa hiyo, hii ina maana kwamba tuongeze kasi ya kuwanasa na kuiondoa hii rushwa katika jamii yetu. Hili ni suala la kila mmoja wetu hapa na vyombo vipo tuvisaidie. Mimi naomba hii sheria tuiunge mkono, tusaidiane na pale panapotokea vipengele vya rushwa tusaidiane kuwanasa hawa watu ili tuwe na jamii ambayo ni safi. Pia alizungumzia kwamba ni kwanini tusipeleke *KCMC*, nadhani hili nimeligusia; pia alisema kutakuwa na fidia gani kama kutakuwa na matunzo, unatunza mtoto ambaye sio wako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii ni kujaribu kutoa majibu na haya majibu unawapa watu baada ya kufarakana huko sisi tunakuja kutoa majibu ya kitaalamu. Sasa sio sheria hii tena ianze kutoa adhabu, sisi tunawapa wale waliowatuma kwamba bwana huyu mtoto sio wake ni wa fulani. Huyu ndiye aliyempa mimba huyu; sasa sheria itachukua mkondo wake na nimeambiwa kwamba *the Children Young Persons Act* inashughulikia mambo kama haya na ni moja ya sheria ambazo nimesema tutazihuisha.

Ninadhani hiyo pia inajibu wazo lake la kwamba kiwepo kipengele kinachosema hawa wanaowapa mimba watoto shuleni wafanywe nini? Kuna sheria ambazo zinahusika, kama tulivyosema, kuna sheria tisa ambazo itabidi vipengele ambavyo vinatambua kwamba *DNA* inaweza ikasaidia katika utekelezaji wa hizo sheria, basi vitumike vipengele hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwalyosi alizungumzia habari za *collector*, nadhani nimelijibu na kwamba tuwe na utaratibu ambao ni wazi. Isiwe kwamba ni *prerogative* ya yule *sampling officer* na hii alikuwa anazungumzia kipengele Na.33 ambacho kinasema *the sampling Officer shall call the sample for human DNA to be transported to the laboratory through the means he may consider appropriate and safe.*

Nakubaliana na haya, maana yake kama ulivyosema anaweza akaenda kwa pikipiki, labda tungesema *through appropriate and safe means* na lisiwe suala la yeye kuamua asafirishe kwa namna gani. Suala la *disposal* kwamba tuna sheria kama ya *NEMC* ambayo inagusa mambo kama haya, nikubaliaane naye kwamba katika sheria ambazo tungezihuisha pamoja na hii ya *DNA*, basi na *NEMC* pia tuiongeze itakuwa ni sheria ya 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu ambao wameandika, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, amezungumzia habari kwamba hizi maabara zisambazwe nchi nzima. Hili suala nimelijibu, ni kwamba wananchi washirikishwe na wapate taarifa. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kabisa kwamba tutatumia kila vyombo kama ilivyo desturi, vipeperushi, redio, TV, ili wajue kuna huduma kama hii ambayo inaweza ikasaidia katika maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Merice Emmanuel, anazungumzia habari ya watu wanaozaliwa na jinsia mbili na kwamba kipimo hiki kitasaidia kutizama ipi ni zaidi. Kama ni mbili moja inakuwa ina *overwhealm* nyingine, kwa hiyo, akawa anashauri kwamba majibu yatoke haraka. Tutajitahidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naulizwa kwamba ni kweli kipimo hiki kitabaini ukweli wa mtu aliyehusika kwa uhakika? Hiki kipimo kwa kutumia mazingira yaliyokuwepo kitasema kwamba huyu alikuwepo katika maeneo yale na hasa ndivyo kinavyotumika. Pia angependa Wizara iongeze vituo vya kuchukulia vipimo hivi na hili nimeshalizungumzia.

Mheshimiwa mwenyekiti, naona nimemaliza, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ambapo nimeweza kutoa majibu kwa haraka haraka. Yanaweza yakawa hayakuwa na mpangilio mzuri lakini ni kwa sababu nilikuwa sijapanga makaratasi yangu vizuri. Lakini hili suala tutaendelea kujadiliana na Wabunge wenzangu na nilichokuwa naomba tu ni kwamba tutakapoingia kwenye vifungu, kuna *spelling mistakes* na *mistakes* ambazo zinaweza zikawa *corrected* na mhariri, kwa hiyo, nilikuwa naomba hivyo visituchulie muda mwingi wakati tunapopita kwenye vifungu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona hoja imetolewa na imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kwa muda huu tuliobakiwa nao nadhani nikiangalia pia jedwali la marekebisho na limegawiwa jioni hii kwa Waheshimiwa. Ninaona hapa kuna *statement* pia ya Mheshimiwa Waziri kwamba kuna vidosari vingi katika uandikaji. Nafikiri nitumie Kanuni Na.28(5), tupate nafasi nzuri ya kuangalia jedwali hili la marekebisho na sheria yenyewe kama ilivyoandikwa ili tuwe na nafasi ya kupitisha sheria hii kiukamilifu siku ya kesho na sio leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninasema hivyo kwa sababu tukiangalia sheria hii kwa haraka tunaweza tukafikiri ni sheria tu fulani ndogo ya kawaida. Lakini kwa kweli inabeba kabisa dhana ya haki za binadamu katika utekelezaji wake.

Kwa hiyo, ninaamini tunatakiwa kuwa na muda wa kutosha ili tuweze kujiridhisha vizuri tutakapokuwa tunaipitisha rasmi kifungu kwa kifungu na hivyo kama nilivyosema kwa Kanuni Na.28(5) ninapata ruhusa ya kuweza kumaliza shughuli hizi. Lakini vilevile kabla sijamaliza shughuli za leo kuna tangazo nimepokea kutoka kwenye meza ya katibu wa Bunge na ninaomba niwasomee kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, kuna nafasi wazi katika maeneo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukituma uwakilishi. Nitasoma tangazo hilo ambalo linawaomba Waheshimiwa Wabunge, wanaofikiri wangependa kuliwakilisha Bunge letu katika maeneo hayo nitakayoyataja, basi wawahi katika Ofisi ya Katibu wa Bunge ili

waweze kuchukua fomu na chaguzi za nafasi hizo zitafanyika tarehe 30 Aprili, siku ya Alhamisi. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Kuna nafasi ya uwakilishi katika Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili, kuziba nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Rwilomba Kabuzi, kwa hiyo, hiyo ni nafasi moja. Lakini vilevile kuna nafasi ya uwakilishi kwenye Baraza la Uongozi la *APRM* nafasi iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Dokta Wanyancha baada ya kuteuliwa kuwa Naibu Waziri.

Kwa hiyo, hiyo nayo ni nafasi moja. Waheshimiwa Wabunge, mtu anayefikiria kugombea huko anaweza kuchukua fomu. Nafasi ya tatu Waheshimiwa Wabunge, ni ya kuwakilisha Bunge la Afrika, kuziba nafasi iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Kabuye, baada ya Mahakama kumvua Ubunge wake. Kwa hiyo, nafasi hiyo pia nayo ni moja na ninadhani kwa utaratibu unaoeleweka, basi tunatoa nafasi ya anayeona anaweza kutuwakilisha huko akaomba.

Katibu wa Bunge anaomba Waheshimiwa Wabunge, wachukue fomu za kugombea katika Ofisi ya Katibu wa Bunge. Narudia kusema kwamba uchaguzi wa nafasi hizo utafanyika tarehe 30 April, siku ya Alhamisi, hapa ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa mujibu wa ratiba itakavyokuwa imepangwa.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa shughuli ya jioni na niwashukuru kwa michango yenu mbalimbali ya kuweza kuimarisha hoja hii ya Muswada huu mpya wa sheria. Baada ya shughuli hizi za leo, sasa naahirisha shughuli zetu za Bunge. Tutakutana kesho saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi huu.

*(Saa 1.14 Usiku, Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 22 Aprili, 2009 saa 3.00 Asubuhi)*